# UELEWA UNAOKUSUDIWA KWENYE SUNNA ZA MTUME


MAANDALIZI

**DR. MOHAMMAD MUKHTAR JUMA**

WAZIRI WA WAQFU
MWANYEKITI WA BARAZA KUU LA MAMBO YA KIISLAMU
NA MJUMBE WA JOPO LA UTAFITI WA KIISLAMU

Kimefasiriwa Na:

Dr. Aiman Al-Asar

Mwalimu Kitivo cha Ufasiri na Ukalimani – Kitengo cha Masomo ya Lugha za Afrika Chuo Kikuu cha Al-Azhar

Mwl. Fadhili Mansour Swaleh.

Mwalimu Kitivo cha Ufasiri na Ukalimani – Kitengo cha Masomo ya Lugha za Afrika Chuo Kikuu cha Al-Azhar.

Mwl. Seifu Seleman Kibwana.

Mwalimu Kitivo cha Ufasiri na Ukalimani – Kitengo cha Masomo ya Lugha za Afrika Chuo Kikuu cha Al-Azhar.



CHAPA YA PILI

2018 / 1440.

Shirika Kuu la Vitabu la Misri.

Shirika Kuu la Vitabu la Misri.

**Mkurugenzi Mkuu.**

**Dr. Haitham Al-Haj Ally**

# UELEWA UNAOKUSUDIWA KWENYE SUNNA ZA MTUME

MAANDALIZI

**DR. MOHAMMAD MUKHTAR JUMA**

**WAZIRI WA WAQFU**

Chapa ya kwanza

Shirikika Kuu la Vitabu la Misri 2021.

S.L.P235 Ramsis

1194 Kornesh Nail – Ramlatu Bolaq Cairo.

Namba ya Post: 11794.

Simu: 202257775109 ndani 149

Fax: 20225764276.

Uchapishaji na utekelezaji

Kituo cha uchapishaji Shirika kuu la Vitabu nchini Misri

Mitazamo iliyopo ndani ya kitabu si msimamo wa shirika bali ni msimamo wa mtunzi kwa hatua ya kwanza.

Haki ya uchapishaji inalindwa na Shirika Kuu la vitabu la Misri. Ni marufuku kuchapisha au kusambaza au kutoa kopi au kuiga kwa hali yeyote ile isipokuwa kwa ruhusa ya Shirika Kuu la Vitabu la Misri au kwa maelekezo ya pande husika.

الفهم المقاصدي سواحيلي

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

﴿**Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anachokukatazeni**﴾ jiepusheni nacho

KWA JINA LA MWENYEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

# UTANGULIZI

Namshukuru Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe wote, sala na salamu ziwe kwa Mitume wake wa mwisho naye ni Mtume Muhammad Ibn Abdillah, pamoja na watu wa nyumbani kwake Maswahaba wake na wenye kufuata uongofu wake mpaka siku ya malipo.

**Baada ya utangulizi huo**:

Wapo baadhi ya watu ni wenye kusimama kwenye maelezo ya wazi ya maandiko lakini hawawezi kuvuka kwenye uwazi wa kazi yake na kufahamu makusudio na malengo yake, wanaingia kwenye ubishi na matatizo wao wenyewe na kwa wale wanaojaribu kuwabebesha uelewa na ufahamu huu ulioganda pasi ya kuwa na ujuzi na

uelewa wa fiqih na kufahamu makusudio ya Sunna Takatifu za Mtume SAW kutokana na kubeba sura nyingi za hekima na wepesi, lau tungekuwa na uelewa mzuri wa Sunna hizi na kuzieleza kwa watu basi tungebadilisha sura hiyo mbaya ambayo imesababisha uelewa na tafasiri zenye makosa kwa makundi ya kigaidi na misimamo mikali. Mwenyezi Mungu amrehemu Al-Hassan Al-Baswary pale aliposema: "Hakika watu wametaka ibada na wakaacha elimu mwishowe wakatoka kwenye uma wa Mtume Muhammad SAW kwa panga zao, lau wangetaka elimu basi wasingekuwa katika hilo" hivyo sisi tunahitaji mafundisho ya Kidini yenye mwangaza yanayojikita kwenye ufahamu wa makusudio makuu ya Sharia ya kati na kati.

Wanachuoni wamesisitiza umuhimu wa uelewa wa makusudio makuu ya uwekaji Sharia, kwani ni mizani ya kina ambayo inaleta udhibiti wa fat'wa na mwenendo wa uboreshaji mazungumzo ya Kidini, wanachuoni wengine wamesisitiza kuwa hukumu katika ujumla wake zimejen-

gwa kwenye kuvuta maslahi au kuondoa uharibifu au yote mawili kwa pamoja.

Kama vile wamesisitiza kuwa miongoni mwa masilahi ni pamoja na kuhifadhi makusudio ya Sharia, na makusudio ya Sharia kwa viumbe ni matano, nayo ni kulinda Dini yao nafsi zao akili zao kizazi chao na mali zao, kila kinachojumuisha kulinda ulinzi wa asili hizi tano kinazingatiwa ni maslahi, na kila kinacho haribu asili hizi tano huo ni uharibifu na huondoa maslahi.

Hakuna shaka kuwa makusudio makuu ya Sunna za Mtume yanafungamana na makusudio makuu ya Qurani Tukufu, kwa kufahamu makusudio ya Qurani na Sunna tutakuwa tumesimama kwenye makusudio makuu ya Dini yetu ya kati na kati, nayo bila ya shaka ni Dini yenye uadilifu wote, huruma zote, usamehevu wote, wepesi wote, ubinadamu na utu wote, wanachuoni wa zamani na wa sasa wanasisitiza kila yanapofikiwa malengo haya makubwa basi huo ni katika mfu-

mo wa Uislamu, na yanayogongana nayo kwa kweli yanagongana na Uislamu pamoja na malengo yake makusudio yake na maumbile yake safi ya usamehevu.

Tunaona wanachuoni wetu wakubwa wakipitisha idadi kadhaa ya misingi na makusudio makuu kwa kuleta kanuni mbalimbali za Kisharia kama vile kauli: ﴾**Mambo kwa makusudio yake**﴿ na ﴾ **Mabadiliko ya hukumu hayapingani na mabadiliko ya zama**﴿ pia ﴾**Asili katika mambo ya manufaa ni halali na asili katika mambo ya madhara ni uharamuna** ﴾**Hakuna kudhuru wala kujidhuru**﴿ pia ﴾**Madhara huondoshwa**﴿ na ﴾**Madhara hayaondoshwi kwa madhara ya mfano wake au zaidi yake**﴿ pia ﴾**Anabeba jukumu la madhara binafsi ili kuondoa madhara kwa uma**﴿ na ﴾**Madhara makubwa huondoshwa kwa madhara mepesi**﴿ pia ﴾**Masilahi ya Umma hutangulizwa dhidi ya masilahi binafsi**﴿ na ﴾**Kuondoa uharibifu kunatangulizwa dhidi ya ku-**

**leta masilahi**﴾ na ﴿**Usiondoe uhabirifu mdogo kwa kupoteza masilahi makubwa**﴾ pia ﴿**Pindi kunapotokea mgongano wa madhara mawili huondolewa gumu kwa jepesi**﴾ na ﴿**Uzito huleta wepesi**﴾ pia ﴿**Dharura uhalalisha vilivyokatazwa**﴾ na ﴿**Kilichohalalishwa kwa dharura hukadiriwa kwa kiwango chake**﴾ pia ﴿**Kawaida uhukumu**﴾ na ﴿**Kinachofahamika hutambulika kama vile kilichowekewa sharti huwa sharti**﴾ na ﴿**Ovu haliondolewi kwa ovu kubwa zaidi**﴾ pia ﴿**Uyakini hauondoki kwa shaka**﴾. Masuala yote yanayokuwa nje na uadilifu na kuwa uovu, yaliyokuwa nje ya huruma na kuwa kinyume chake, yaliyokuwa nje ya masilahi na kuwa uharibifu, yaliyokuwa nje ya busara na kuwa ni uchafu, basi yote hayo si kitu chochote kwenye Sharia.

Sisi wenye hitajio kubwa la kusoma na kufahamu makusudio ya Sunna za Mtume zinazofuatana na roho ya zama za sasa na mambo yake mapya na kuwa karibu Sunna za Mtume kwa watu badala ya ufahamu na ufafanuzi wenye kuwa-

kimbiza watu kwenye Sunna za Mtume bali hata kwenye Dini yenyewe wala hawawi karibu nayo wala yenyewe kuwa karibu na wao.

Katika wigo huu kitabu hiki kinakuja ili kufungua mlango upya mbele ya usomaji na jitihada za kisasa kwenye Sunna Tukufu za Mtume SAW zinazofanywa na wanachuoni wenye weledi, jitihada ambazo zinachunga hali na mabadiliko ya nyakati na maeneo pamoja na hali za watu wakiweka macho yao kwenye yale yaliyoamuliwa na wasomi wa misingi ya mambo ya Dini na wanafiqhi kuwa fat'wa hubadilika kwa kubadilika wakati na sehemu au hali za watu au hali za wanafat'wa wenyewe, na kuwa zile hoja zilizopewa nguvu ndani ya zama fulani kutokana na kukubaliana na masilahi ya wakati huo huenda hoja hizo zikawa hazina nguvu ndani ya zama zengine ikiwa hali ya zama hiyo imebadilika na kubadilika sura ya masilahi, kwani yenye kutolewa fat'wa ndani ya zama fulani kwenye mazingira fulani na katika hali fulani huenda ndani ya zama nyengine ikawa ni bora

zaidi kutolewa fat'wa ikiwa zama zimebadilika au mazingira yamebadilika au hali zimebadilika madamu tu yote hayo yapo katika wigo wa dalili za Kisharia zinazo zingatiwa na makusudio makuu ya Sharia, na ikawa fat'wa hizo zimetolewa na mtu au watu wa jitihada na mtazamo.

Nimejaribu kuonesha baadhi ya mifano ya kiutendaji katika kusoma maandiko ya Mtume SAW ikiwa ni kuangaza na kuandaa njia ya utafiti zaidi katika mwelekeo huu, kwa makadirio ya chini nimeangalia umuhimu wa kufikiri na kuifanyisha kazi akili wakati wa kusoma maandiko Sunna sahihi na uthibiti wake, pamoja na kutofautisha kati ya kuangalia andiko na yale yaliyoandikwa miongoni mwa sherehe au ufafanuzi mdogo wa pembeni au mtazamo jumla, wala hatuipi sherehe utakatifu wa andiko asili wala mabadiliko kuyavesha nguo thabiti.

Ni mataraji yangu kuwa nimeyafikia yale niliyokusudia na kutoa mchango katika kuanga-

zia kadhia muhimu za kuleta mabadiliko mapya kwenye mazungumzo ya Kidini.

Mwenyezi Mungu yupo nyuma ya kusudio na Yeye ndiyo muwezeshaji na msaidizi.

***Dr. Muhammad Mukhtari Juma Mabrouk***

Waziri wa Waqfu

Mwenyekiti wa Baraza Kuu la Mambo ya Kiislamu

Na mjumbe wa Jopo la watafiti wa mambo ya Uislamu la Azhari Al-Sharif.

## UTAFITI WA KWANZA.

## MAZUNGUMZO YA QURANI TUKUFU KUHUSU MTUME S.A.W

Qurani Tukufu imezungumza kuhusu Mtume SAW kwa mazungumzo yanayoelezea nafasi yake Mtume maadili yake na mambo mengi yanayofungamana na Mtume SAW, kwani Yeye ni Mtume wa huruma ambapo Mwenyezi Mungu wa Kweli Anasema: ﴿**Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote**﴾ [1].

Anasema tena Mola Mtukufu: ﴿**Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungelikuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangelikukimbia. Basi wasamehe, na**

(1) Al- Anbiyaa: 107

**waombee maghfira, na shauriana nao katika mambo. Na ukisha kata shauri basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wanao mtegemea﴾[1].**

Anasema tena Mola: ﴿**Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutaabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma﴾ [2].**

Pia Anasema tena Mola: ﴿**Na jueni kuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu yuko nanyi. Lau angeli kutiini katika mambo mengi, bila ya shaka mungelitaabika. Lakini Mwenyezi Mungu amekupendezeeni Imani, na akaipamba katika nyoyo zenu, na amekufanyeni muuchukie ukafiri, na upotovu, na uasi. Hao ndio waliooongoka﴾** [3].

(1) Aal-Imraan: 159.
(2) At-Tawbah: 128.
(3) Al- Hujraat: 07.

Mola Ameutakasa ulimi wa Mtume wake na Akasema: ﴿**Wala hatamki kwa matamanio**﴾ (1).

Akayatakasa macho ya Mtume wake na Akasema: ﴿**Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka**﴾ (2).

Akatakasa moyo wake na Akasema: ﴿**Moyo haukusema uwongo uliyo yaona**﴾ (3).

Akaitakasa akili yake na kusema: ﴿**Mwenzenu huyu hakupotea, wala hakukosea**﴾(4).

Akatakasa ufahamu wake na Akasema: ﴿ **Amemfundisha aliye mwingi wa nguvu**﴾(5)**.**

Akatakasa tabia zake na kusema: ﴿**Na hakika wewe una tabia tukufu**﴾ (6).

---

(1) An-Najmu: 03.
(2) An-Najmu: 17
(3) An-Najmu: 11
(4) An-Najmu: 02
(5) An-Najmu: 05
(6) Al-Qalam: 04

Akamtakasa kama alivyo kwa kusema: ﴿**Hakika nyinyi mnayo ruwaza njema kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa anaye mtaraji Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho, na akamkumbuka Mwenyezi Mungu sana**﴾ (1).

Akakunjua kifua chake na Akasema: ﴿**Hatukukunjulia kifua chako?**﴾ (2).

Akamsamehe makosa yake yaliyotangulia na yatakayo kuja na Akasema: ﴿**Hakika tumekufungulia Ushindi wa wazi * Ili Mwenyezi Mungu akusamehe makosa yako yaliyotangulia na yajayo, na akutimizie neema zake, na akuongoe katika Njia Iliyo Nyooka**﴾ (3).

Akafanya kumuunga mkono kwake Mtume SAW ni uungaji mkono wa Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Bila ya shaka wanao fungamana nawe,**

---

(1) Al-Ahzab: 21
(2) As-Sharh: 01
(3) Al-Fathu: 1-2

**kwa hakika wanafungamana na Mwenyezi Mungu. Mkono wa Mwenyezi Mungu uko juu ya mikono yao. Basi avunjaye ahadi hizi anavunja kwa kuidhuru nafsi yake; na anaye tekeleza aliyo muahidi Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atamlipa malipo makubwa﴾** [(1)].

Akawakanya watu wanaoinua sauti zao mbele ya Mtume SAW Akasema Mola Mtukufu: **﴿Enyi mulio amini! Musinyanyue sauti zenu kuliko sauti ya Nabii, wala musiseme naye kwa kelele kama munavyosemezana nyinyi kwa nyinyi, visije vitendo vyenu vikaharibika, na hali hamtambui﴾**[(2)].

Akawasifu watu wenye kushusha sauti zao mbele ya Mtume SAW Akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: **﴿Kwa hakika wanao teremsha sauti zao mbele ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, hao ndio Mwenyezi Mungu amezisafisha nyoyo zao**

(1) Al-Fat'hu: 10
(2) Al-Hujraat: 02

**kwa ucha-Mungu. Hao watakuwa na msamaha na malipo mkubwa﴾[1].**

Akayafanya maisha ya Mtume SAW ni ulinzi kwa Umma wake badala ya kuwapa adhabu za haraka Akasema Mola Mtukufu: ﴿**Na Mwenyezi Mungu hakuwa wa kuwaadhibu nawe umo pamoja nao, wala Mwenyezi Mungu si wa kuwaadhibu na hali ya kuwa wanaomba msamaha**﴾[2].

Pindi Mtume SAW aliposoma kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu kupitia ulimi wa Nabii Ibrahimu AS: ﴿**Ewe Mola wangu Mlezi! Hakika hayo yamewapoteza watu wengi. Basi aliye nifuata mimi huyo ni wangu, na aliye niasi, hakika Wewe ni Mwenye kusamehe Mwenye kurehemu**﴾ [3].

**Na kauli yake Mola Mtukufu kupitia ulimi wa Nabii Issa AS: ﴿Ukiwaadhibu basi hao ni**

(1) Al-Hujraat: 03
(2) Al-Anfaal: 33.
(3) ibrahimu: 36

**waja wako. Na ukiwasamehe basi Wewe ndiye Mwenye nguvu na Mwenye hikima﴾ [1].**

Mtume SAW aliinua mikono yake huku akilia na kusema: "Ewe Mwenyezi Mungu Umma wangu Umma wangu. Akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: Ewe Jibril, nenda kwa Muhammad – Mola wako anajua zaidi – na muulize kitu gani kinacho kuliza, malaika Jibril akaja kwa Mtume SAW na akamuuliza na kumuelezea aliyosema Mwenyezi Mungu kuwa Yeye anajua zaidi. Mwenyezi Mungu akasema: Ewe Jibril nenda kwa Muhammad na mwambie: Hakika tutakuridhisha kwa ummati wako na wala hatutakufanyia ubaya" [2], ambapo Anasema Mola Mtukufu: ﴿**Na Mola wako Mlezi atakupa mpaka uridhike**﴾ [3].

(1) Al-Maidah: 118

(2) Kitabu cha sahihi Muslimu kwenye - Kitabu cha Iman – mlango wa maombi ya Mtume SAW kwa Umma wake, na kulia kwake kwa kuuonea huruma Umma wake, Hadithi nambari 2020: Imehakikiwa na Muhammad Fuad Abdulbaaq, chapa ya Dar Ihyaau Turaath al-Araby, Beirut.

(3) Ad-dhuhaa: 05.

Mola wake amemkirimu hata katika kumzungumzia na kumwita kwake, ambapo Mola Mtukufu amewaita Mitume wengine kwa majina yao: ﴿**Na tulisema: Ewe Adam! Kaa wewe na mkeo katika Bustani**﴾ [1].

Akasema tena Mola Mtukufu: ﴿**Ikasemwa: Ewe Nuhu! Shuka kwa amani itokayo kwetu, na baraka nyingi juu yako na juu ya watu walio pamoja na wewe**﴾ [2].

Akasema Mola wa haki: ﴿**Tulimwita: Ewe Ibrahim! * Umekwisha itimiliza ndoto**﴾[3].

Akasema tena Mola Mtukufu: ﴿**Ewe Daudi! Hakika Sisi tumekufanya wewe uwe Kiongozi katika nchi**﴾ [4].

Akasema tena: ﴿**Basi alipo ufikia akaitwa: Ewe Musa * Hakika Mimi ndiye Mola wako**

---

(1) Al-Baqarah: 35.
(2) Huud: 48
(3) Swaaffaat: 104 – 105.
(4) Swaad: 26.

**Mlezi! Basi vua viatu vyako. Kwani upo katika bonde takatifu la T'uwa﴾** [1].

Amesema tena Mwenyezi Mungu: ﴿**Ewe Zakariya! Hakika Sisi tunakubashiria mwana; jina lake ni Yahya﴾** [2].

Pia akasema: ﴿**Ewe Yahya! Kishike Kitabu kwa nguvu! Nasi tulimpa hekima angali mtoto﴾** [3].

Pia akasema tena: ﴿**Na pale Mwenyezi Mungu atapo sema: Ewe Isa Ibn Maryamu! Kumbuka neema yangu juu yako, na juu ya mama yako**[4].

Mwenyezi Mungu Mtukufu amemzungumzia Mtume wetu SAW uzungumzaji uliokutana na heshima ya Ujumbe au Utume au sifa au ukarimu na ubora, akasema Mola Mtukufu: ﴿**Ewe Mtume!**

(1) Twaha: 11-12.
(2) Mariamu: 07
(3) Mariamu: 12
(4) Al-Maidah: 110

**Fikisha uliyo teremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi﴾** [1].

Na akasema: ﴿**Ewe Nabii! Hakika Sisi tumekutuma uwe shahidi nambashiri na mwonyaji﴾** [2].

Akasema tena Mola Mtukufu: ﴿**Ewe uliye jifunika!* Kesha usiku kucha, ila kidogo tu! * Nusu yake, au ipunguze kidogo﴾**[3].

Akasema tena Mola Mtukufu: ﴿**Ewe uliye jigubika! * Simama uonye! * Na Mola wako Mlezi mtukuze! * Na nguo zako, zisafishe﴾**[4].

Pindi Mola alipompa heshima kwa kutaja jina lake ndani ya Qurani Tukufu alilitaja kwa kukutanisha na utukufu wa Ujumbe, akasema: ﴿**Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na walio pamoja naye wana nguvu mbele ya makafiri, na wanahurumiana wao kwa wao﴾**[5].

---

(1) Al-Maidah: 67.
(2) Al-Ahzaab: 45.
(3) Al-Muzzammil: 1 - 3
(4) Al-Muddaththir: 1 - 4
(5) Al-Fat'hi: 29.

Akasema Mola wa Haki: ﴿**Na Muhammad hakuwa ila ni Mtume tu. Wamekwishapita kabla yake Mitume**﴾(1).

Akachukua ahadi kwa Manabii na Mitume kuwa watamwamini na kumtetea, akasema Mola wa Haki: ﴿**Na pale Mwenyezi Mungu alipo chukua ahadi kwa Manabii: Nikisha kupeni Kitabu na hekima, kisha akakujieni Mtume mwenye kusadikisha muliyo nayo, ni juu yenu mumuamini na mumsaidie. Akasema: Je, mumekiri na mumekubali kushika agizo langu juu ya hayo? Wakasema: Tumekubali. Akasema: Basi shuhudieni, na Mimi ni pamoja nanyi katika kushuhudia**﴾(2).

Miongoni mwa ukarimu wake Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa Mtume SAW ni kuufanya ujumbe wake kuwa ni wa watu wote, ambapo ilikuwa kila Mtume akitumwa kwa watu wake tu, ama kipenzi

(1) Aal-Imraan: 144.
(2) Aal-Imraan: 81

chetu Mtume Muhammad SAW Mwenyezi Mungu Mtukufu amemtuma kwa watu wote, akasema Mola Mtukufu: ﴿**Na hatukukutuma ila kwa watu wote, uwe mbashiri, na mwonyaji**﴾[(1)].

Akafanya Ujumbe wake kuwa Ujumbe wa mwisho, naye Mtume SAW akamfanya ndio mwisho wa Manabii na Mitume, akasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii**﴾[(2)].

Naye Mtume SAW ni mlinganiaji wa baba wa Manabii Ibrahimu SA na mbashiriwa wa Nabii Issa AS ambapo anasema Mtume SAW: "Mimi ni mlinganiaji wa baba yangu Ibrahimu na bishara ya Nabii Issa kwa watu wake, na mtazamo wa mama yangu ambaye aliona kuwa imetoka kwake nuru iliyoangazia majumba ya Shamu" [(3)]. Na hilo Anas-

(1) Sabai: 28.
(2) Al-Ahzaab: 40.
(3) Kitabu cha Imamu Ahmad 28/395 namba 17163: Chapa ya

ema Mola Mtukufu kupitia ulimi wa Nabii Ibrahimu AS: ﴿**Ewe Mola Mlezi wetu! Waletee Mtume anayetokana na wao, awasomee Aya zako, na awafundishe Kitabu na hekima na awatakase. Hakika Wewe ndiye Mwenye nguvu, Mwenye hekima**﴾[1].

Pia Anasema kupitia ulimi wa Nabii Issa AS: ﴿**Na Isa bin Mariamu alipo sema: Enyi Wana wa Israili! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu, ninaye thibitisha yaliyo kuwa kabla yangu katika Taurati, na mwenye kubashiria kuja Mtume atakaye kuja baada yangu; jina lake ni Ahmad! Lakini alipo waletea hoja zilizo wazi, walisema: Huu ni uchawi uliowazi!**﴾[2].

Naye Mtume SAW ni muombezi wa kwanza na wa kwanza kupewa uombezi kwa Umma wake,

---

Taasisi ya Risalah.
(1) Al-Baqarah: 129.
(2) As-Swaff: 06.

naye ndiye mwenye sehemu nzuri inayosifika siku ya kiyama, ambapo Anasema Mola Mtukufu: ﴿**Na amka usiku kwa ibada; ni ziada ya Sunna khasa kwako wewe. Huenda Mola wako Mlezi akakunyanyua cheo kinacho sifika**﴾[1].

Mwenyezi Mungu mwenyewe amekuwa ni mwenye kumshushia sala zake na kuwaamrisha Malaika pamoja na Waumini wamsalie Mtume SAW pale Aliposema: ﴿**Hakika Mwenyezi Mungu na Malaika wake wanamsalia Nabii. Enyi mlio amini! Msalieni na mumsalimu kwa salamu**﴾[2].

Na akaifanya sala yake kwa Waumini ni rehema na utulivu kwao, Akasema Mola Mtukufu: ﴿ **Na uwaombee rehema. Hakika maombi yako ni utulivu kwao. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia Mwenye kujua**﴾[3].

(1) Al-Israa: 79.
(2) Al-Ahzaab: 56.
(3) At-Tawbar: 103.

Mwenyezi Mungu akafanya sala zao kwa Mtume ni mlango mpana wa maombezi yake SAW kwao siku ya kiyama, ambapo anasema Mtume wetu SAW: "Pindi munapomsikia muadhini basi semeni kama anavyosema, kisha nisalieni kwani mwenye kunisalia sala moja SAW basi kwa sala hiyo anamalipo kumi, kisha niombeeni kwa Mwenyezi Mungu wasila kwani ni sehemu ndani ya pepo isiyopaswa isipokuwa kwa mja katika waja wa Mwenyezi Mungu na ninategemea mimi kuwa ndio mja mwenyewe, basi mwenye kuniombia mimi hiyo wasila mtu huyo itakuwa halali kwake kupata uombezi wangu" [1].

****

(1) Hadithi inapatikana kwenye kitabu cha Sahihi Muslimu, kitabu cha sala mlango wa kauli inayopendeza mfano wa kauli ya muadhini kwa mwenye kumsikia. Hadithi namba 384.

## UTAFITI WA PILI:

## NAFASI YA SUNNA NA HOJA ZAKE.

Pindi tunapozungumza kuhusu Sunna za Mtume SAW huwa tunazungumzia chanzo cha pili cha Sharia ya Kiislamu, wanachuoni kwa ujumla wao wamekubaliana juu ya hoja ya Sunna ya Mtume na kuwa kumtii Mtume SAW ni katika kumtii Mwenyezi Mungu Mtukufu, ambapo Mola Mtukufu Anasema: ﴿**Enyi mlio amini! Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume na wenye madaraka katika nyinyi. Na mkizozana katika jambo basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa munamuamini Mwenyezi Mungu na Siku ya Mwisho. Hayo ndiyo bora zaidi na ndiyo yenye mwisho mwema**﴾[1].

(1) An-Nisaa: 59.

Anasema tena Mola Mtukufu: ﴿**Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume ili mpate kurehemewa**﴾[1].

Pia Anasema: ﴿**Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume. Na wakigeuka basi Mwenyezi Mungu hawapendi makafiri**﴾[2].

Anasema tena Mola Mtukufu: ﴿**Na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala musizozane mukaingiwa woga na zikapotea nguvu zenu. Na subirini. Hakika Mwenyezi Mungu yupo pamoja na wanao subiri**﴾[3].

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Na mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume, na tahadharini. Na ikiwa mutageuka basi jueni ya kuwa jukumu la Mtume wetu ni kufikisha ujumbe tu ulio wazi**﴾[4].

(1) Aal-Imraan: 132.
(2) Aal-Imraan: 32.
(3) Al-Anfaal: 46.
(4) Al-Maidah: 92.

Anaema tena Mwenyezi Mungu: ﴿**Sema: Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume. Na mkigeuka, basi yaliyo juu yake ni aliyo bebeshwa, na yaliyo juu yenu ni muliyo bebshwa nyinyi. Na mkimtii yeye mtaongoka. Na hapana juu ya Mtume ila kufikishaUjumbe wazi wazi**﴾[1].

Anasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Mwenye kumtii Mtume basi ndio amemtii Mwenyezi Mungu. Na anaye kengeuka, basi Sisi hatukukutuma wewe uwe ni mlinzi wao**﴾[2].

Anasema tena Mwenyezi Mutukufu: ﴿**Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, hao wapamoja na wale alio waneemesha Mwenyezi Mungu miongoni mwa Manabii, na Masiddiqi, na Mashahidi, na Watu wema. Na uzuri ulioje kuwa pamoja na watu hao * Hiyo ni fadhila itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kutosha**﴾[3].

(1) An-Nuur: 58.
(2) An-Nisaau: 80.
(3) An-Nisaau: 69-70

Na Anasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Na anaye mtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, bila ya shaka amefanikiwa mafanikio makubwa**﴾(1).

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Hiyo ni mipaka ya Mwenyezi Mungu. Na anaye mtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, Yeye atamtia katika Pepo zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Na huko ndiko kufuzu kukubwa**﴾(2).

Anasema tena Mwenyezi Mungu: ﴿**Na mwenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, atamuingiza katika Mabustani yapitayo mito kati yake. Na atakaye geuka upande atamuadhibu kwa adhabu chungu**﴾(3).

Anasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿ **Haiwi kauli ya Waumini wanapo itwa kwa Mwe-**

(1) Al-Ahzaab: 71.
(2) An-Nisaau: 13.
(3) Al-Fat'hu: 17.

**nyezi Mungu na Mtume wake ili ahukumu baina yao, ila nikusema: Tumesikia na tumetii! Na hao ndio wenye kufanikiwa * Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na wakamwogopa Mwenyezi Mungu na wakamcha, basi hao ndio wenye kufuzu﴾**[1].

Mwenyezi Mungu Anasema tena: ﴿**Na hatukumtuma Mtume yeyote ila atiiwe kwa idhini ya Mwenyezi Mungu. Na lau pale walipo jidhulumu nafsi zao wangeli kujia, wakamwomba Mwenyezi Mungu msamaha, na Mtume akawaombea msamaha, hapana shaka wangeli mkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba na Mwenye kurehemu﴾**[2].

Mwenyezi Mungu Anasema tena: ﴿**Na anacho kupeni Mtume chukueni, na anachokukatazeni jiepusheni nacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu﴾**[3].

********

(1) An-Nuur: 51-52.
(2) Ani-Nisaau: 64.
(3) Al-Hashri: 07.

Qurani Tukufu inasisitiza umuhimu wa kuteremka kwenye hukumu ya Mtume SAW katika maisha yake na kwa muktadha wa Sunna zake Takatifu katika maisha yake na baada ya kufa kwake SAW ambapo Mwenyezi Mungu Anasema: ﴿**La! Naapa kwa Mola wako Mlezi! Hawataamini mpaka wakufanye wewe ndiye muamuzi katika yale wanayo khitalifiana, kisha wasione uzito katika nyoyo zao juu ya hukumu utayo toa, na wanyenykee kabisa**﴾[1].

Na Anasema tena Mola Mtukufu: ﴿**Haiwi kwa Muumini mwanamume wala Muumini mwanamke kuwa na hiyari katika jambo, Mwenyezi Mungu na Mtume wake wanapo kata shauri katika jambo lao. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi**﴾[2].

***

(1) An-Nisaa: 65.
(2) Al-Ahzaab: 36.

Mwenyezi Mungu Mtukufu Amekataza na kutahadharisha kwa mwenye kwenda kinyume na amri ya Mtume SAW Akasema: ﴿**Basi watahadhari wanao kwenda kinyume na amri yake, usije ukawapata msiba au ikawapata adhabu chungu**﴾[(1)].

Anasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Enyi mlio amini! Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume, wala musiviharibu vitendo vyenu**﴾[(2)].

Akasema tena Mwenyezi Mungu: ﴿**Enyi mlio amini! Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala musijiepushe naye, nanyi munasikia * Wala musiwe kama wale wanao sema: Tumesikia na kumbe hawasikii * Hakika wanyama waovu mbele ya Mwenyezi Mungu ni waile viziwi na bubu wasio tumia akili zao * Na Mwenyezi Mungu angeli jua wema wowote**

(1) An-Nuur: 63.
(2) Muhammad: 33.

**kwao angewasikilizisha, na lau ange wasikilizisha wangeli geuka wakapuuza﴿**[1].

Anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴾**Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake basi hakika amepotea upotofu ulio wazi**﴿[2].

Anasema tena Mwenyezi Mungu: ﴾**Na anaye muasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, na akaipindukia mipaka yake, (Mwenyezi Mungu) atamtia Motoni adumu humo, na atapata adhabu ya kudhalilisha**﴿[3].

Anasema tena Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴾**Na wenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake, basi hakika hao watapata Moto wa Jahannamu wadumu humo milele**﴿[4].

Mwenyezi Mungu akatubainishia wazi kuwa kila maelekezo yanayotoka kwa Mtume SAW basi

(1) Al-Anfaal: 20 -23.
(2) Al-Ahzaab: 36.
(3) An-Nisaa: 14.
(4) Al-Jinni: 23.

ni ufunuo aliofunuliwa, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: ﴿**Naapa kwa nyota inapo tua * Mwenzenu huyu hakupotea, wala hakukosea * Wala hatamki kwa matamanio * Hayakuwa haya ila ni ufunuo ulio funuliwa**﴾[1].

Na Mtume SAW kwa hakika anatulingania kwenye yale yanayotupatia uhai, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: ﴿**Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tutakusanywa**﴾[2].

Mwenyezi Mungu Akafanya utiifu kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu na kufuata Sunna zake SAW ni sababu ya kupata radhi za Mola Mtukufu na mapenzi yake, pamoja na kupata msamaha wa dhambi, Amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu:

(1) An-Najmu: 1 – 4.
(2) Al-Anfaal: 24.

﴿**Sema: Ikiwa nyinyi munampenda Mwenyezi Mungu basi nifuateni mimi, Mwenyezi Mungu atakupendeni na atakufutieni madhambi yenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kufuta madhambi na Mwenye kurehemu**﴾[1].

Anasema Mtume wetu SAW: "Je kuna mtu anafikisha Hadithi kuhusu mimi hali ya kuwa amekaa sehemu yake na akasema: Kati yetu na nyinyi ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu, yale tutakayoyakuta kuwa halali basi tunayahalalisha, na tukiyakuta yaliyo haramu tutayaharamisha, kwani alichoharamisha Mtume wa Mwenyezi Mungu ni kama alichoharamisha Mwenyezi Mungu" [2]. Anasema Mtume SAW: "Nilinganienі yale niliyokuachieni, hakika wameangamia wale waliokuwa kabla yenu kwa kuuliza kwao na kutofautiana

(1) Aal-Imraan: 31.

(2) Sunan ya Tirmidhy – Kitabu cha mambo ya elimu, mlango unaokataza imesemwa kwa upande wa Hadithi ya Mtume SAW, ni Hadithi namba 2664 uhakiki na maelezo ni: Ahmad Muhammad Shaakir, usambazaji ni: Shirika la maktaba na uchapishaji la Mustafa Al-Baaby Al-Halaby, Misri, chapa ya pili 1395H – 1975.

na Mitume wao, pindi ninapokukatazeni kitu basi kuweni nacho mbali, ikiwa nitawaamrisha jambo basi lifanyeni vile munavyoweza"[1]. Anasema tena Mtume wetu SAW: "Umma wangu wote utaingia peponi isipokuwa kwa yule aliyekataa, akaulizwa Mtume, ni nani atakayekataa ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: ﴿Mwenye kunitii mimi ataingia peponi na mwenye kuniasi mimi basi huyo atakuwa amenikataa"[2].

Kutoka kwa Abdillah Ibn Abbas RA amesema Mtume SAW: ﴿Enyi watu nimekuachieni jambo ikiwa mutashikamana nalo basi hamtapotea kabisa: Ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu na Mwenendo wa Mtume wake﴾ [3]. Kutoka kwa Al-a'rbaadh

(1) Kitabu cha sahihi Bukhary – Kitabu cha kushikamana na Qurani pamoja na Sunna, mlango wa kufuata Sunna za Mtume SAW,.Hadithi namba 7288, uhakiki: Muhammad Zuel Ibn Nasir An-Nasir, usambazaji: Dar Twauk An-Najaat, chapa ya kwanza 1422H.
(2) Hadithi imo kwenye kitabu cha Sahihi Al-Bukhary – Kwenye maudhui iliyopita, Hadithi namba 7280.
(3) Hadithi inapatikana kwenye kitabu Al-Mustadriku 1/171 Hadithi namba 318 Dar al-kutub al-ilmiyah, Beirut.

Ibn Saariyah RA: Hakika Mtume SAW amesema: "Ninakuusieni kumcha-Mwenyezi Mungu, kusikiliza na kutii hata kama msemaji atakuwa ni mtu wa kihabeshi, yeyote miongoni mwenu mwenye kuishi baada yangu na akaona tofauti nyingi basi ni juu yenu kuangalia mwenendo wangu na mwenendo wa Makhalifa walioongoka, shikamaneni nao kwa kung'ata kwa meno ya magego, na ole wenu na mambo ya uzushi, kwani kile uzushi ni bida'a na kila bida'a ni upotovu"**(1)**.

Anasema Mtume SAW: "Mwenye kwenda kinyume na mwenendo wangu basi huyo si katika mtu wangu"**(2)**. Anasema tena Mtume SAW: "Mwenye kunitii mimi basi atakuwa amemtii Mwe-

---

(1) Kitabu cha Sunani za Abi Daud – Kitabu cha Sunna, mlango wa ulazima wa Sunna, Hadithi namba 4607, Uhakiki: Muhammad Muhyddeen AbdulHameed, usambazaji: Maktaba ya Asiliya. Beirut.

(2) Kitabu cha Sahihi Bukhary – Kitabu cha mambo ya ndoa – mlango wa upendezeshaji wa ndoa, Hadithi namba 5063, na ndani ya kitabu cha Sahihi Muslimu – Kitabu cha mambo ya ndoa – mlango wa yanayopendeza kwenye ndoa kwa mwenye kujiamini na kupata uwezo wa kugharamia ndoa, Hadithi namba 1401.

nyezi Mungu, na mwenye kuniasi mimi atakuwa amemuasi Mwenyezi Mungu"[1].

Amesema Ibn Abbas RA: Aya tatu zimeteremka zikiwa zimekutana na mambo matatu, jambo moja haliwezi kukubalika bila ya jengine, ya kwanza: Ni kauli yake Mola Mtukufu: ﴿**Mtiini Mwenyezi Mungu, na mtiini Mtume**﴾[2]. Mwenye kumtii Mwenyezi Mungu pasi ya kumtii Mtume wake utiifu wake hautokubalika, ya pili: Kauli ya Mwenyezi Mungu: ﴿**Na shikeni Sala, na toeni Zaka**﴾[3]. Mwenye kusali bila ya kutoa zaka haitokubalika sala yake, ya tatu: Ni kauli ya Mola Mtukufu: ﴿**Nishukuru Mimi na wazazi wako**﴾[4]. Mwenye kumshukuru Mwenyezi Mungu pasi ya

(1) Sahihi Bukhary kitabu cha hukumu mlango wa kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: {Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume pamoja na wenye mamlaka miongoni mwenu﴾Hadithi namba 7137 na kitabu cha Sahihi ya Imamu Muslimu kitabu cha mambo ya uongozi mlango wa wajibu wa kuwatii viongozi katika mambo yasiokuwa ya maasi, hadithi namba 1835.
(2) An-Nisaa: 59.
(3) Al-Baqarah: 43.
(4) Luqman: 14.

kuwashukuru wazazi wake basi shukrani zake hazitokubaliwa. Kwa sababu hiyo amesema Mtume SAW: "Radhi za Mwenyezi Mungu zipo kwa kuwaridhisha wazazi wawili, na hasira za Mwenyezi Mungu zipo kwa kuwachukiza wazazi wawili"[(1)].

Amenukuliwa Ibn Rajab Al-Hambaly [(2)] kutoka kwa Imamu Ahmad Ibn Hambal [(3)] kuwa

---

(1) Sehemu ya Imani Hadithi inayotokana na Baihaqy 6/177 mlango katika kuwafanyia wema wazazi wawili. Hadithi namba 7830 chapa ya Dar al-Kutubu al-Al-ilmiya, Beirut.

(2) Ni Abul-Faraj Zeynuddeen Abdulrahman Ibn Ahmad Ibn Rajabu As-Salaamy Al-Baghdady, amekuwa maarufu kwa jina la Ibn Rajabu Al-Hambaly, alizaliwa mwaka wa 736H, ni mwenye kuhifadhi Hadithi, amafikia kiwango cha kuwa Imamu katika fat'wa zake, ni katika wanachuoni wa madhehebu ya Imamu Ahmad Ibn Hambaly, miongoni mwa vitabu vyake muhimu alivyotunga ni pamoja na: Jaamii al-uluum wal-hikamu, na kitabu Latwaaif al-Maarif, alifariki Damscus nchini Syria mwaka wa 795H historia hii inapatikana kwenye kitabu cha Al-Aalaam cha Zarkaly 3/295, kinasambazwa na Dar al-alamu lil malaayeen, chapa ya kumi na tano ya mwaka 2002.

(3) Ni Abu Abdillah Ahmad Ibn Muhammad Ibn Hambal As-Shaibaany Ad-Dhahly, alizaliwa huko Baghdady nchini Iraq mwaka wa 164H, ni mmoja wa Maimamu wanne kwa watu wa Sunna na Jamaa, ndio mwenye madhehebu ya Al-Hambaly katika Fiqhi ya Kiislamu, alifariki mwaka wa 241H, historia hii

amesema: Asili ya Uislamu upo kwenye Hadithi tatu: Hadithi iliyopokelewa na Omar RA: Mtume SAW anasema: "Hakika matendo yanakwenda kwa nia". Na Hadithi iliyopokelewa na Bibi Aisha RA. Mtume SAW amesema: "Mwenye kuzusha kitu kwenye hili jambo letu ambacho hakimo basi kitu hiko kinarudishwa﴾. Na Hadithi iliyopokelewa na An-Nu'umaan Ibn Basheer RA. Mtume SAW anasema: ﴿Halali ipo wazi na haramu ipo wazi"(1).

Kutoka kwa Aby Daud As-Sajastaany (2) amese-

---

inapatikana kwenye kitabu cha Seir Aalaam An-Nablaa cha shamsuddeen Ad-Dhahaby, alifariki mwaka wa 748 – 11/177. Uhakiki: Umefanywa na jopo la wahakiki kwa usimamizi wa Sheikh Shuaibu Al-Arnaauutw, kimesambazwa na: Taasisi ya Ar-Risalah, chapa ya tatu ya mwaka 1405H sawa na mwaka 1985.

(1) Maelezo yanayopatikana kwenye kitabu cha Jami'I al-uluum wal-Hikam cha Ibn Rajabu Al-Hambaly 1/61 chapa ya Dar – Al-Maarifah – Beirut.

(2) Ni Imamu Abu Daud, Suleiman Ibn Al-Ash'ath Ibn Is'haq Ibn Basheer Al-Azdy As-Sajastaany, Imamu wa watu wa Hadithi katika zama zake, asili yake ni kutoka Sajastan, ni mwenye kitabu cha As-Sunan nacho ni moja ya vitabu sita vya Sunna, alifariki huko Basrah mwaka wa 275H, maelezo haya yanapatikana kwenye kitabu cha Seir A'alaam An-Nablaa 13/203 chapa ya Ar-Risaalah, na pia kwenye kitabu cha Al-A'alam cha Zarkaly 3/122.

ma: Fiqh inazunguka kwenye Hadithi tano: "Halali ipo wazi na haramu ipo wazi". Na kauli ya Mtume SAW: "Hakuna kuleta madhara wala kujidhuru". Na kauli yake Mtume SAW: "Matendo yanakwenda kwa nia". Pia kauli yake Mtume SAW: "Yale niliyowakataza kwayo basi jiepusheni nayo". Na kauli yake SAW: "Yale niliyowaamrisheni kwayo basi yatekelezeni kiasi muwezavyo"[(1)].

Wala haiwezi kuletewa mjadala nafasi ya Sunna Takatifu za Mtume na hoja zake pamoja na ukubwa wa nafasi yake isipokuwa kwa mtu mpingaji au mbishi asiyezoelekea kwa kauli yake, kwani wasomi wanakubaliana kuwa Sunna Takatifu za Mtume SAW ni chanzo cha pili cha Sharia ya Kiislamu, hivyo kumekuwa na uangalizi wa hali ya juu, katika kuhifadhi mapokezi uandishi ukokotoaji ushereheshaji na utoaji wa hukumu, tofauti na misimamo ya baadhi ya wenye ufahamu mdogo kwenye maandiko pasi ya kufahamu makusudio

(1) Jaami'I Al-Uluum wal-Hikam cha Ibn Rajabu Al-Hambaly ukurasa wa 62.

yake hupelekea mgando wa kifikra na kupotea kwenye kadhia nyingi, jambo ambalo linaifanya Hadithi kwenye uelewa wa makusudio ya Sunna za Mtume SAW kuwa ni jambo muhimu sana na kuhitajika sana ili kuvunja mgando na upotoshaji wa kifikra.

Hakuna shaka kuwa Sunna zimekuja kusherehesha na kubainisha pamoja na kukamilisha Quran Tukufu. Anasema Mola Mtukufu: ﴿**Nasi tumekuteremshia wewe Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyo teremshwa kwao, wapate kufikiri**﴾(1).

Na Anasema tena Mola Mtukufu: ﴿**Na Mwenyezi Mungu amekuteremshia Kitabu na hikima na amekufundisha uliyokuwa huyajui. Na fadhila za Mwenyezi Mungu zilizo juu yako ni kubwa**﴾(2).

Anasema Tena Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Yeye ndiye aliye mpeleka Mtume kwenye**

(1) An-Nahli: 44.
(2) An-Nisaa: 113.

**watu wasiojua kusoma, awasomee Aya zake na awatakase, na awafunze Kitabu na hekima, ijapo kuwa kabla ya haya walikuwa katika upotofu ulio dhaahiri﴾**[1].

Anasema Mola Mtukufu: ﴿**Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu juu yenu, na aliyo kuteremshieni katika Kitabu na hekima anacho kuonyeni kwacho. Na mcheni Mwenyezi Mungu, na jueni kwamba hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu﴾**[2].

Anasema pia Mola Mtukufu: ﴿**Na kumbukeni yasomwayo majumbani mwenu katika Aya za Mwenyezi Mungu na hekima. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mambo ya siri, na Mwenye habari﴾**[3].

Al-Hassan Al-Baswary [4] pamoja na Imamu

(1) Al-Jum'aa: 02
(2) Al-BAqarah: 231.
(3) Al-Ahzaab: 34.
(4) Ni Al-Hassan Ibn Yasaar Al-Baswary ni katika watu wa Taabii, alikuwa Imamu kwa watu wa Basrah na msomi wa Umma ka-

Shaafy [1] na wengineo miongoni mwa wanachuoni na wanachuoni wa tafasiri wamesema kuwa hekima hapa ni Sunna za Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW [2].

Wamezungumza wanachuoni wa masomo ya asili ya Dini kuhusu hoja za Hadithi kwa mapana zaidi, anasema Imamu Shaafy RA: Mwenyezi Mungu Mtukufu amemuweka Mtume wake SAW katika Dini yake na amri zake pamoja na Kitabu chake sehemu ambayo amebainisha - Mola Mtukufu – kuwa amemfanya kuwa ni alama ya Dini yake katika ulazima uliowekwa wa utiifu wake

---

tika zama zake, alifariki mwaka wa 110H, historia hii inapatikana kwenye kitabu cha Al-Aalaam cha Zarkaly 2/226.

(1) Ni Abu Abdillah Muhammad Idris Shaafy Al-Qurashy, ni Imamu wa tatu katika Maimamu wanne wa watu wa Sunna na makubaliano ya wanachuoni, ni mwenye madhehebu ya Shaafy na muasisi wa elimu ya asili ya Fiqhi, alizaliwa Gazzah mwaka wa 150H. Miongoni mwa utunzi wake ni pamoja na kitabu cha Al-Ummu na Ar-Risaalah, ni kitabu cha kwanza cha aina ya elimu ya asili ya Fiqhi, alifariki nchini Misri mwaka wa 204H. Angalia kitabu Al-Aalaam cha Zarkaly 6/26.

(2) Rejea hayo: Tafasiri ya Twabary na Ibn Katheer na wengineo kwenye Aya ya 129 ya Surat Al-Baqarah.

Mola Mtukufu, na kuharamisha kumuasi, na akabainisha ubora wake kwa kukutanisha kumuamini Mtume wake SAW na kumuamini Yeye, akasema Mola Mtukufu: ﴿**Hakika Waumini ni wale walio muamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake tena wasitie shaka kabisa, na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali yao na nafsi zao. Hao ndio wa kweli**﴾[1].

Akafanya ukamilifu wa kuanza kwa Imani unafuatana na kumuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, ikiwa mja atamuamini Mwenyezi Mungu pasi ya kumuamini Mtume wake basi mja huyo hatokuwa na jina la Imani kamilifu mpaka aamini Mtume wake pamoja na Yeye Mwenyezi Mungu [2].

Na anasema RA: Sijamsikia yeyote watu wakimnasibisha au akijinasibisha yeye mwenyewe kwenye elimu inayokwenda kinyume katika kufaradhisha Mwenyezi Mungu Mtukufu kufuata

(1) Al-Hujraat: 15.
(2) Kitabu cha Ar-Risaalah cha Imamu Shaafy, kimefanyiwa uhakiki na: Sheikh Ahmad Shaakir 1/75 chapa ya Dar Al-Kutub al-Ilmiyah – Beirut.

amri za Mtume wa Mwenyezi Mungu na kukubali hukumu yake kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu hakumfanya yeyote baada ya Mtume isipokuwa ni mfuasi wa Mtume, na kuwa mfuasi hyo halazimiki na kauli kwa hali yeyote isipokuwa ni kwa Kitabu cha Mwenyezi Mungu au Sunna za Mtume wake SAW na visivyokuwa hivyo vinatokana na Kitabu na Sunna, na amri ya kufaradhisha Mwenyezi Mungu kwetu na kwa watakao kuja baada yetu na wale waliokuwepo kabla yetu katika kukubali habari itakayo kwa Mtume SAW ni moja [(1)].

Na anasema Ibn Hazmu[(2)] RA: Ndani ya Qurani ipi imeelezwa kuwa Swala ya Adhuhuri ina rakaa nne, Magharibi rakaa tatu, na kurukuu kunatakiwa

---

(1) Kitabu cha Al-Ummu cha Imamu Shaafy – ni kitabu kilichokusanya elimu kubwa 7/287 chapa ya Dar al-Maarifah, Beirut.

(2) Abu Muhammad Ally Ibn Ahmad Ibn Said Ibn Hazmu Al-Andulus Al-Qurtwubay, miongoni mwa wanachuoni wa Andulus, miongoni mwa utunzi wake ni pamoja na kitabu cha: Al-Mahally, mlango katika Mila mapenzi ya nafsi na tamaduni, ikiwa ni hukumu katika asili za hukumu. Alifariki mwaka wa 456H sawa na mwaka 1064. Kitabu Al-Aalaam cha Zarkaly 4/254.

kuwe namna hii, kusujudu kunatakiwa kuwa hivi, sifa ya usomaji ndani ya Swala na utoaji wa salamu mwisho wa Swala, na kubainisha yanayopaswa kuwanayo mbali wakati wa kufunga, pamoja na kubainisha namna ya utoaji wa Zaka ya dhahabu na madini ya fedha, wanyama aina ya mbuzi na kondoo ngamia na ng'ombe, na kiwango cha idadi inayochukuliwa kwa wanyama hao kwenye utoaji wa Zaka, ubainifu wa matendo ya ibada ya Hijja kuanzia wakati wa kusimama viwanja vya Arafah, kuswali Muzdalifah, urushaji wa vijiwe, namna ya kuhirimia hijja pamoja na kufahamu yanayopaswa kuwa nayo mbali wakati wa utekelezaji wa ibada ya Hijja, utekelezaji wa adhabu ya kukatwa mkono mwizi, sifa ya unyonyeshaji ulioharamishwa, na vyakula vilivyo haramu kuliwa, sifa ya uchinjaji na udhuhiya, hukumu za adhabu za jinai, sifa ya kutoka talaka, hukumu za uuzaji, maelezo kuhusu riba, utoaji wa sadaka na aina zengine mbali mbali za Fiqhi? Kwa hakika ndani ya Quran Tukufu kuna jumla ikiwa tutaachwa na jumla hizo tu basi hatutafahamu ni namna gani tutazifanyia kazi, lakini

marejeo yake katika yote hayo ni kunukuu kutoka kwa Mtume SAW[1].

Anasema As-Shaukany[2] RA: Fahamu kuwa wamekubaliana watu wa elimu Sunna Takatifu ni zenye kujitegemea katika kuweka Sharia za hukumu, na yenyewe ni kama Quran Tukufu katika kuhalalisha yaliyo halali na kuharamisha yaliyo haramu, imethibiti kutoka kwa Mtume SAW kuwa amesema: "Fahamu mimi nimepewa Quran pamoja na mifano wake»[3] kwa maana nimepewa Quran na nimepewa mfano wake miongoni mwa Sunna ambazo hazikuzungumzwa na Quran, na hilo ni kama mfano wa kuharamishwa kila aina ya

(1) Kitabu cha hukkumu katika asili za hukumu cha Ibn Hazmu 2/79 Dar Al-Aafaaq al-Jadidah - Beirut.

(2) Muhammad Ibn Ally Ibn Muhammad Ibn Abdillah As-Shaukany, ni mwanachuoni mwenye jitihada katika wanachuoni wakubwa wa Yemen, katika utunzi wake ni pamoja na kitabu cha Nail Al-Autwar, Fathu Al-Qadeer, alifariki huko Swana'a nchini Yemen mwaka wa 1759H – 1834. Angalia kitabu Al-Aalaam cha Zarkaly 6/298.

(3) Ni Hadithi iliyopokelewa na Imamu Ahmad katika kitabu chake 28/410 Hadithi nambari: 17174.

wanyama wakali wenye kuwinda kwa kwa meno na jamii ya ndege wenye kuwinda kwa kutumia kucha, na yasiyo kuwa hayo ambayo idadi yake ni kubwa"[1].

Anasema: Jumla ni kuwa kuthibiti kwa hoja ya Sunna zilizotakasika na kujitegemea kwake katika kuweka Sharia za hukumu ni jambo muhimu katika Dini, wala hakuna anayekwenda kinyume na hivyo isipokuwa kwa yule mtu asiyekuwa na nafasi katika Dini ya Uislamu[2].

Anasema Al-Aaluusy[3] RA: ﴿**Mtiini Mwenyezi**

(1) Kitabu cha Irshaad al-Fuhuul ilaa tahkik al-hakk, ni kitibu cha aina za elimu za asili ya Fiqhi cha Shaukany 1/96 chapa ya Dar al-Kitabu Al-Araby.
(2) Chanzo kilichopita kuelezewa.
(3) Mahmuod Shihabuddeen Al-Aaluusy, ikiwa ni kunasibishwa na Mji wa Alusy nao ni Kisiwa kilichopo katikati ya mto wa Furat ndani ya mkoa wa Al-ambaar, ni mfasiri, mtu wa Hadithi, mwana fiqhi, mtu wa fasihi na mshairi, alikuwa Mufti wa mji wake mwaka wa 1248H, kisha akasafiri kwa ajili ya kusoma zaidi, miongoni mwa utunzi wake: Tafasiri Ruuh Al-Maany, alifariki mwaka 1803 – 1854. Angalia kitabu Al-Aalaam cha Zarkaly 7/172.

**Mungu**﴾ kwa maana: Lazimikeni na utiifu kwake katika yale aliyokuamrisheni nayo na kuwakatazeni nayo. ﴿**Mtiini Mtume**﴾ aliyeletwa ili kufikisha hukumu zake kwenu katika kila anachokuamrisheni nacho na kuwakatazeni pia, na kurejea kitenzi – Ikiwa utiifu kwa Mtume umekutanishwa na utiifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu – ni kuinua nafasi ya Mtume SAW na dalili ya wazi kwa wenye kudhani kuwa hakuna kufuata zaidi ya Quran, na ruhusa kuwa Mtume SAW amekuwa na utiifu wa pekee ambao haujathibiti kwa mwengine [1].

Anasema Mwalimu Abdulwahaab Khalaf[2] RA:

(1) Kitabu cha Ruuh Al-Maany fii tafseer Al-Quran, cha Al-Aaluusy 5/65 chapa ya Dar Ihyaau Turaath Al- Araby – Beirut.

(2) Ni mwanachuoni wa Fiqhi na mjumbe katika jopo la wataalamu wa lugha ya Kiarabu jijini Cairo, alizaliwa mwaka 1888 ni mwenye vitabu vingi alivyovitunga hasa katika elimu ya asili ya Fiqhi, aliteuliwa hakimu wa mahakama za Kisharia mwaka 1920 kisha akawa Mkurugenzi mkuu wa Misikiti ya Wizara ya Waqfu mwaka 1924 na kubakia katika wadhifa huo mpaka akateuliwa kuwa mkaguzi wa mahakama za Kisharia katikati ya mwaka wa 1931, akawa mwalimu wa Chuo Kikuu cha Cairo kitivo cha masomo ya haki akiwa mwalimu wa kufundisha

Sunna ima iwe ni Sunna yenye ufafanuzi na kufasiri yale yaliyokuja ndani ya Quran kwa sifa ya jumla, au iwe yenye kujifunga katika yale yaliyokuja moja kwa moja au iwe na sifa maalumu kwa yale yaliyokuja kwa sura ya wote, hivyo inakuwa ufasiri huu au kujifunga huku au umaalumu huu ambao umekuja kwenye Sunna ni ubainifu wa kusudio la yaliyokuja ndani ya Quran, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu amempa Mtume wake SAW haki ya kubainisha maandiko Aya za Quran kwa kauli yake: ﴿**Nasi tumekuteremshia wewe Ukumbusho ili uwabainishie watu yaliyo teremshwa kwao, wapate kufikiri**﴾[(1)].

Kutokana na haya: Sunna ambazo zimefafanua namna ya utekelezaji wa ibada ya Swala, ibada ya utoaji Zaka na ibada ya Hijja, ni kwa sababu Quran

---

mwanzoni mwa mwaka 1934, na kubakia kuwa mwalimu wa Sharia ya Kiislamu mpaka akafikia umri wa kustaafu mwaka 1948, alifariki mwaka 1375H. Angalia ufasiri wake wa utangulizi wa kitabu chake ﴿Asili ya elimu ya Fiqhi na ufupisho wa historia ya utengenezaji Sharia﴾ ukurasa wa 3.

(1) An-Nahli: 44.

imeamrisha kutekeleza ibada za Swala na kutoa Zaka pamoja na kutekeleza ibada ya Hijja lakini haikupambanua idadi ya rakaa za Swala, wala viwango vya Zaka, wala mifumo ya ibada za Hijja, hivyo Sunna za vitendo na kauli ndizo ambazo zimefafanua amri hii iliyokuja kwa ujumla wake ndani ya Quran, vile vile Mola Mtukufu Anasema: ﴾**Lakini Mwenyezi Mungu ameihalalisha biashara na ameiharamisha riba**﴿[1].

Na Sunna ndio ambayo imebainisha uuzaji sahihi na ule uuzaji mbaya uliyo haramu, na kuelezea aina za riba zilizo haramishwa. Mwenyezi Mungu ameharamisha mzoga, na Hadithi au Sunna ndizo ambazo zimebainisha kusudio ukiacha mzoga wa baharini, na yasiyo kuwa hayo miongoni mwa Sunna ambazo zimebainisha na kufafanua kusudio la ujumla wa Quran na uwazi wake na ujumla wake, hivyo Sunna inazingatiwa ni kamilisho la Quran na ambatano lake [2].

(1) Al-Baqarah: 275.
(2) Elimu ya Asili ya Fiqhi, kitabu cha Abdulwahaab Khalaf ukurasa wa 40 chapa ya Matwbaatul madany – Misri.

Na kwa kufuata msingi wa yote yaliyotangulia katika Aya za Quran Tukufu na Sunna za kipenzi Mtume Muhammad SAW pamoja na kauli za Wanachuoni inatuwia wazi makubaliano ya wanachuoni juu nafasi kubwa ya Sunna za Mtume SAW, na juu ya hoja zake zenye kufafanua na kufasiri pamoja na kubainisha na kukamilisha, hakuna anayeweza kuleta mjadala katika hilo isipokuwa ni mtu mpingaji mkaidi na mbishi, au mtu asiye na nafasi katika elimu, wala kuzoeleka mtazamo wake kwa watu wa mazingatio na mtazamo.

***

## UTAFITI WA TATU:

## ULAZIMA WA MITAZAMO MPYA.

Hakuna shaka kuwa kupiga hatua mbele kwenye kuleta mitazamo mipya katika uelewa na kuelezea kadhia za kifiqh, pamoja na kuangalia mambo mapya ya zama na baadhi ya kadhia zenye kukubali kufanyiwa jitihada, kuna hitaji mtazamo uelewa na ufahamu wa kina wenye ushujaa na uthubutu uliopangiliwa, pamoja na makadirio mazuri ya mambo ndani ya wakati mmoja.

Kama vile kunahitajika kwa mwenye kufanya kazi hiyo kuwa na nia safi kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu ikiwa ni pamoja na yatakayo msaidia kuwa na ufahamu mzuri na kuvumilia ukosoaji na mshale wenye kuchoma kwa wale waliofunga mlango wa jitihada, na wakaapa kwa kiapo chao kikubwa kuwa Umma haukuzaa na wala hautozaa

hapo baadaye mwana jitihada, na kuwa Umma huu umekuwa ni tasa utasa usio na tiba, wakiwa wamesahau au kutokujua kuwa Mwenyezi Mungu Mtukufu hakuhusisha elimu wala elimu za Sharia kwa watu pasi ya watu wengine au kwa zama pasi ya zama zengine, na kuwa heri katika Umma wa Mtume Muhammad SAW zitaendelea mpaka siku ya kiyama,

Ili tukatize njia kuepukana na nyongeza zozote basi mimi ninasisitiza juu ya uthibiti na mambo yafuatayo:

Yaliyothibiti kwa dalili ya moja kwa moja na yale yaliyokubaliwa na Umma na yakawa ni yenye kufahamika katika Dini kwa umuhimu wake kama vile asili ya Imani faradhi za Uislamu miongoni mwa ulazima wa ibada ya Swala ibada ya Funga ibada ya Zaka na kuhiji kwenye Kaaba kwa mwenye uwezo wa kuelekea, yote hayo hakuna sababu ya kutofautiana katika hayo, ni mambo ya lazima yaliyowekwa hayabadiliki kwa kubadilika wakati au sehemu au hali na watu, eneo la kuleta

jitihada ni kila hukumu ya Kisharia isiyo na dalili ya moja kwa moja, anasema Imamu Abu Haamid Al-Ghazaly[(1)] RA katika kitabu chake cha Al-Mustaswfy: Wajibu wa Swala tano pamoja na ibada za Zaka na yale waliyokubaliana Wanachuoni wa Umma miongoni mwa mambo ya wazi ya Sharia yakiwa na dalili ya moja kwa moja basi anapata dhambi yule mwenye kuwa kinyume na mambo hayo, kwani hakuna nafasi ya kufanya jitihada katika mambo hayo[(2)].

1- Sisi tunaangalia kwa makadirio yote pamoja na kuheshimu mitazamo ya Umma wa wanajiti-

(1) Abu Hamid Muhammad Ibn Muhammad Al-Ghazaly aliyefariki mwaka wa 505H ni mwanafalsafa mtu wa tasaufi ana vitabu kiasi cha mia mbili alivyotunga mwenyewe, aliitwa kwa jina la ﴾Hoja ya Uislamu﴿, miongoni mwa vitabu vyake muhimu alivyotunga ni pamoja na: Ihyaau Uluumiddeen, Al-Iqtiswaad fil Itiqaad, kimafanyiwa uhakiki na Dr.Mahmoud Twanahy, kimesambazwa na: Ofisi ya Hijr ya uchapishaji na usambazaji, chapa ya pili 1413H, angalia kitabu Al-Aalaam cha Zarkaly 7/22.

(2) Kitabu cha Al-Mustaswfy cha Ibn Hamid Al-Ghazaly ukurasa wa 345, kimefanyiwa uhakiki na: Muhammad Abdulsalaam Abdulshaafy, chapa ya Dar al-Kutub Al-ilmiyah.

hada kwa mfano: Imamu Abi Hanifah, Imamu Malik, Imamu Shaafy, Imamu Ahmad na wale wote waliokuwa mfano wao miongoni mwa Wanachuoni na Wanasharia wanaozingatiwa katika jitihada zao, tunaona kuwa wote hao ni Wanachuoni na wenye ubora mkubwa, kwani kila mmoja wao amefanya kazi kubwa ya kuleta jitihada na kuelewa katika wigo wa mazingira ya zama zake, na Umma ukapokea madhehebu yao kwa ridhaa na kukubali.

2- Pia tunaamini kuwa baadhi ya fat'wa zilikubaliana na zama zao muda wao na sehemu zao, au hali za wanafat'wa, na yale yaliyopewa nguvu ndani ya zama zao sawa na muktadha wa masilahi ya ndani ya wakati huo yanaweza kuwa yana nguvu ndani ya zama zengine ikiwa hali za zama hiyo zimebadilika na kubadilika sura ya masilahi, na yale yanayotolewa fat'wa ndani ya zama fulani katika mazingira fulani na katika wigo wa hali fulani huenda yakawa katika zama zengine ni bora zaidi katika fat'wa

ikiwa hali ya zama itabadilika, au kubadilika mazingira au hali madamu yote hayo ni katika wigo wa dalili ya Kisharia inayozingatiwa, na makusudio makuu ya Sharia madamu jambo limetolewa fat'wa kutoka kwa mtu au watu wa jitihada na mtazamo.

Imamu Al-Quraafy [(1)] RA ametaja katika kitabu chake cha hukumu kuwa: Inapaswa kwa Mufti pindi anapopata habari ya kuwepo mtoa fat'wa pasi ya kujua kuwa ni mtu wa nchi hiyo hiyo ambaye yeye Mufti yumo, hivyo asitoe fat'wa kwa mazoea yake ya kutoa fat'wa mpaka amuulize kuhusu mji wake, je imekuwa inafahamika katika mji huo kwa tamko hili au hapana?

3- Sisi tunaamini rai na rai ya mwengine, na kwa uwezekano wa kuwa ni rai sahihi katika baadhi

(1) Abu Abbas: Shihabudeen Ahmad Ibn Idris al-Maaliky maarufu kwa jina la Al-Quraafy, mwenye utaifa wa Misri na kukulia Misri pia amefia Misri, ana utunzi wa vitabu vya Fiqhi na asili ya Fiqhi, alifariki mwaka wa 684H. angalia kitabu cha Al-Aalaam cha Zarkaly 1/95.

ya kadhia zenye tofauti, katika wigo wa hali ya uwepo wa fat'wa nyingi na matukio yake pamoja na tangulizi zake, ikiwa baadhi ya waliotutangulia katika waja wema wamesema: Rai yangu iliyo sahihi kuna uwezekano wa kuwa na makosa na rai yangu yenye makosa inawezekana ikawa sahihi, sisi tunakwenda mbali zaidi na tunasema: Hakika rai zote mbili zinaweza kuwa ni sahihi, ispokuwa rai moja itakuwa na nguvu zaidi na nyengine itakosa nguvu, tunaichukua ile tunayoiona ni yenye nguvu pasi ya kuipa makosa ile tunayoiona haina nguvu, madamu mwenye rai ni katika watu wa jitihada, kwa rai yake ina nafasi ya kuangaliwa na kuwa na dalili ya Kisharia inayozingatiwa, kauli zenye nguvu sio zimezuiliwa kuwa na makosa, na kauli zisizo na nguvu sana sio zenye kuharibu wala kubomolewa.

4- Kasi kubwa ya maisha ya zama za sasa katika pande mbalimbali za kielimu kiuchumi kiteknolojia kuongezea pia mabadiliko na

mashirikiano pamoja na mabadiliko ya kisiasa kiuchumi kimaisha na kijamii, yote hayo yanalazimisha kwa Wanachuoni na Wanasharia kuangalia tena hukumu katika wigo wa mabadiliko yote haya, ili kutoka kwenye wigo wa mgando wa kifikra ambao baadhi ya makundi yenye misimamo mikali yanajaribu kulazimisha mgando huo wa kifikra kupitia kulazimisha mitizamo yao iliyoganda na kujifunga kwenye jamii.

Uislamu umefungua mlango mpana wa jitihada, kwani Mtume wetu SAW amepitisha msingi wa kuleta jitihada hata katika zama za uhai wake SAW, pale Mtume SAW alipomtuma Muadhi Ibn Jabali RA kuelekea nchini Yemen akamuuliza: ﴿Ni vipi utatoa hukumu ikiwa utaletewa kadhia?﴾ akasema Muadhi: NItahukumu kwa kutumia Kitabu cha Mwenyezi Mungu, Mtume SAW akamuuliza tena: ﴿Ikiwa haujapata hukumu yake ndani ya kitabu cha Mwenyezi Mungu?﴾ akasema: Nitahukumu kwa kuangalia mwenendo wa Mtume wa Mwe-

nyezi Mungu SAW. Mtume akamuuliza: ﴿Ikiwa haujapata hukumu katika Sunna na mwenendo wa Mtume wa Mwenyezi Mungu?﴾ akasema: Nitafanya jitihada kwa rai yangu bila kuchoka, anasema Muadhi Mtume SAW akawa ameniwekea mkono wake juu ya kifua changu na akasema SAW: "Namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amemuwezesha mjumbe wa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa lile linalomridhia Mtume wa Mwenyezi Mungu" (1), kusudio la kauli yake "Bila kuchoka" kwa maana ya kuchoka kufanya jitihada na katika kuangalia masuala.

Hakuna shaka kuwa Hadithi hii ya Mtume SAW inazingatiwa ni nguzo katika kufungua mlango wa jitihada na akili kuifanyisha kazi mpaka siku ya mwisho, ambapo ameanza Swahaba Muadhi Ibn Jabal RA kwa kuangalia kwanza kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu kwa maana ya Quran, ikiwa

(1) Kitabu cha Sunani ya Abi Daud – Kewnye kitabu cha hukumu, mlango wa jitihada za rai katika kuhukumu, Hadithi namba 3592.

atakuta masuala yaliyopewa fat'wa yana hukumu ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu atatekeleza sawa na hukumu iliyokuja kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu ni sawa sawa ikiwa ni hukumu ya moja kwa moja yenye kuthibiti na dalili au ikiwa hukumu ya moja kwa moja iliyothibiti dalili ya kidhana, kwa maana yenye kuhitaji kuifanyisha kazi akili katika kutoa hakumu, pamoja na kufikiwa hukumu yenye uhalisia unaoendana na Aya, ikiwa katika masula hayo hajapata Aya ya Quran si yenye dalili ya moja kwa moja wala dalili ya dhana basi ataangalia Sunna za Mtume wa Mwenyezi Mungu ni sawa sawa ikiwa kwa kufasiri Aya ya Quran au kubainisha ujumla wake au kufunga kule kuelezea kwake au kuhusisha ule ujumla wake uliokuja au kuwa kadhia ni ngeni katika kuleta hukumu ya kina katika wigo wa makusudio makuu ya Sharia zilizokusanywa ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu, ikiwa hatopata Aya ya moja kwa moja ya hukumu katika masuala au hajapata Aya kabisa, amekusudia kutumia akili na kupima masuala yenye mfanano na kuleta jitihada ya rai yake pasi ya kuacha kuangalia masuala ya Kisharia.

**Katika hayo tunayo ya kuangalia**:

**La Kwanza:** Muadhi Ibn Jabal RA alikuwa amepelekwa na Mtume SAW nchini Yemen katika zama za uhai wa Mtume SAW wala Muadhi hakusema kumwambia Mtume SAW ikiwa nitakosa hukumu ya masuala ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu Mtukufu wala katika Sunna za Mtume wa Mwenyezi Mungu kuwa nisubiri au nisimame mpaka nirudi kwako Mtume SAW au nimtume mjumbe kuja kwako, na Mtume SAW wala hakumtaka afanye hivyo, bali alimpa uhuru wa kufanya jitihada wakati wa zama za uhai wa Mtume SAW, wala hakumtaka arudi kwake na kumfikishia yale yanayotakiwa kutolewa hukumu, bali alimwachia nafasi kubwa na ya kutosha ya kuleta jitihada zake na mtazamo wake huku Mtume SAW akisema: "Namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amemuwezesha mjumbe wa Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa lile analoridhia Mtume wa Mwenyezi Mungu".

**La Pili:** Mtume SAW amesema: "Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu analeta kwenye Umma huu kila mwisho wa miaka mia moja mtu mwenye kuleta mitazamo mipya ndani ya Dini yake" [(1)], na uasilia wa mitazamo hii mipya haiwi isipokuwa ni kwa njia ya jitihada na mtazamo na kuchunga hali ya zama iliyopo na mambo yake mapya, pamoja na kusoma uhalisia kwa usomaji mpya katika wigo wa makusudio makuu ya Sharia.

**La Tatu:** Maswahaba RA walikuwa ni wenye kufuata mfumo wa Mtume SAW baada ya kuondoka kwake, hapa tunamkuta Omar Ibn Khattab RA anatuma barua yake ya kihistoria ya masuala ya kuhumu kwa Abi Mussa Al-Ash'ary RA, na yalikuwa miongoni mwa yaliyoandikwa ni "Kutoka kwa Abdillah Omar Ibn Khattab, Kiongozi Mkuu wa Waumini kuelekea kwa Abi Mussa Al-Ash'ary: Baada ya utangulizi, hakika kutoa hukumu ni kazi

(1) Hadithi inapatikana kwenye kitabu cha Aby Daud – Kitabu Al-mulaahim, mlango yanayotajwa ndani ya karne moja, ni Hadithi namba 4293.

ya lazima ya Mahakama na ni mwenendo wa kufuatwa, fahamu pindi ukiletewa kadhia basi haifai kuzungumza haki usiyoitekeleza, na waunganishe watu katika vikao vyako na maelekezo yako mpaka asipatwe na tamaa mtu mwenye ukubwa katika msimamo wako wala kukatishwa tamaa mtu mnyonge kwenye uadilifu wako….kuelewa ni kuelewa pindi kifua chako kinapo hangaika katika yale hayajakufikia kutoka kwenye Kitabu cha Mwenyezi Mungu wala Sunna za Mtume SAW, fahamu mifano na mifanano na pima masuala katika mifano hiyo na mifanano hiyo, kisha egemezea hukumu unayoipenda kwa Mwenyezi Mungu na iliyofanana sana na ukweli kwa yale unayo yaona"[(1)].

Omar RA wala hakumtaka Aby Mussa Al-Ash'ry kusimama kutoa hukumu mpaka arejee kwa

(1) Angalia Sunani ya Dar Qutwny – Kitabu katika kadhia na hukumu na yasiyokuwa hayo, maandiko ya Omar kwenda kwa Abi Mussa 4/207 Dar Al-Maarifah – Beirut nchini Lebanon, na kitabu kinachoitwa Iilaam Al-muwaqqeen an Rabbil Aalameen cha Ibn Qiyam Al-Juuziyah 1/85 kimefanyiwa uhakiki na: Twaha Abdulrauf, chapa ya Dar Al-Jabal – Beirut.

Omar RA, kama vile hakumtaka mpaka akusanye watu kwenye masuala, pamoja na hilo kuwa ni jambo lenye kupendezeshwa na Sunna kwa mwenye kuhitaji hivyo, tofauti kuwa msimamizi wa mambo ya dola au mwenye kufanya jitihada huwa anafanya hivyo pindi ikihitajika kwake, pamoja na kusisitiza kwetu juu ya rai ya kiongozi huondoa tofauti kwa wenye kutofautiana kwa masilahi yanayozingatiwa katika wigo wa makusudio makuu ya Sharia ya kati na kati.

5- Lazima tuweke kwenye mazingatio yetu kuwa mabadiliko yeyote au mitazamo mipya katika kuelezea kadhia za mazungumzo ya Kidini katika historia ya mwanadamu haiwezekani kuwa sehemu ya kukubaliana rai za wengi kabla ya kuchagua ongezeko la muda unaokuwa mrefu na ule unaokuwa mfupi sawa na kuridhika kwa wanafikra mpya na misimamo yao pamoja na jitihada zao na uwezo wao wa kukinaisha mitazamo yao ya fikra mpya, na wale waigaji na wenye kuhifadhi pamoja na wanufaikaji na

hali yenye utulivu haiwezekani kujisalimisha kwa haraka na wepesi ambao wanautegemea wanafikra mpya, na kwa kiwango cha akili za wanafikra mpya pasi ya kuwazidishia wale wanaowazingatia kwenda pande zengine za mbali na kuwa maandalizi ya jamii ya kupokea na kukubali fikra zao, kwa kukata kwao njia kwa watu wa fikra zilizoganda na kuwa ngumu kwa kupenda kwao mauaji.

6- Tunasisitiza juu ya fikra mpya ambapo tunafanya juhudi kuziendea ni lazima zisimamiwe kwa mizani ya Sharia na akili, na kutoachwa zikiporwa na watu wasio stahiki na wasio kuwa wa weledi ambao wanataka kubomoa misingi thabiti chini ya madai ya uletaji wa fikra mpya, uwiano wa kina na hatua ya kina kabisa kutokana na kubeba changamoto za ndani na nje, mwenye weledi pindi anapojitahidi na kukosea basi anakuwa na malipo ya aina moja, ikiwa atafanya jitihada na akapatia basi ana malipo ya aina mbili, aina ya kwanza ni malipo ya jitihada

yake na aina ya pili ni malipo ya kupatia kwake, ama mwenye kuthubutu kutoa fat'wa hali ya kuwa hana elimu nayo, ikiwa atapatia basi ana dhambi moja, ikiwa atakosea basi anadhambi za aina mbili, aina ya kwanza ni kule kuvamia kwake jambo asilo na ujuzi nalo, na aina ya pili ni athari inayotokana na makosa yake kwenye jamii na Dini kwa pamoja, ndani ya wakati ambao anahitajika mtu mwenye kujenga na wala sio mwenye kubomoa.

Vile vile tunasisitiza kuwa kugusa misingi thabiti ya Imani na kupinga yaliyothibiti kwenye uelewa wa Umma basi huko ni kunahudumia nguvu ya misimamo mikali pamoja na ugaidi hasa katika wigo wa hali tunayoipitia, kwa sababu makundi ya misimamo mikali yanatumia mfano wa mapungufu kama haya kusambaza misimamo mikali ndani ya misingi hii thabiti, jambo ambalo linapaswa kuangaliwa na kulichukulia tahadhari nalo, ikiwa tunataka kufuta misimamo mikali kutoka kwenye mizizi yake basi ni lazima kwanza ku-

ondoa sababu za mizizi hiyo, kwani kila kitendo kina yake yaliyo sawa na kitendo chenyewe katika makadirio na kinyume chake katika muelekeo, wanasema: Kila kitu kinapande mbili na katikati, ikiwa wewe utashika upande mmoja basi upande wa pili utainama, lakini ikiwa umeshika katikati basi pande zote mbili zitakuwa zipo sawa, hivyo basi amesema Imamu Al-Auzaii[1] RA: "Jambo lolote aliloamrisha Mwenyezi Mungu isipokuwa jambo limepingwa na sheitan kwa sababu mbili pasi ya kujali ni sababu ipi atakuwa amepitia, kuzidisha kwa kupitiliza au upungufu" [2], hivyo sisi tupo pamoja na kutangaza wepesi katika Dini na wala si kutangaza uzito, tupo katika kutangaza usamehevu wa Dini na wala sio Imani ya kupitiliza,

(1) Ni Imamu Haafidh Abu Amru Abdurahman Ibn Yuhmad Al-Auzaii, ni Imamu wa watu wa Shamu ndani ya zama zake, alizaliwa huko Baalabakka mwaka wa 88H, na alikuwa ni miongoni mwa wanachuoni wakubwa wenye kutetea Uislamu na Sunna za Mtume SAW, alifariki nchini Lebanon mwaka wa 157H. Soma kitabu Sair Aalaam An-Nablaa 7/107.

(2) Kitabu cha Al-Maqaaswid Al-Hasanah cha Sakhaawy. Ukurasa wa 332 chapa ya Dar Al-Kutub Al-Araby.

pamoja na kulazimika Kidini na kimaadili pasi ya kuwa na misimamo mikali au mgando wa kifikra au kujifungia kinadharia, kwani kati ya msimamo mkali na kuwajibika Kidini kuna uzi mwembamba sana, na kati ya kufanya wepisi na uzito kuna uzi mwembamba sana, mwenye akili ni mwenye kufahamu tofauti hii nyembamba sana, na anasimama kwenye mpaka wake akiwa ni mwenye uelewa pasi ya kuwa mwenye ujinga, Imamu As-Suyuutwy amenukuu kwenye kitabu chake kinachoitwa Al-Itqaan fii Uluumi Al-Quran[1] kutoka kwa Al-Mauruudy kuwa amesema: Nimemsikia Aba Is-haaq Ibrahim Ibn Mudhaarib Ibn Ibrahim anasema: Nimemsikia baba yangu anasema: Nilimuuliza Hussein Ibn Fadhli na nikasema: Hakika yako wewe unatoa mifano ya Waarabu na Waajemi ndani ya Quran je umeshakuta ndani ya Kitabu cha Mwenyezi Mungu ﴿Ubora wa mambo ni ukati na

(1) Al-Itqaan fii Uluumi Al-Quran cha Imamu As-Suyuutwi 4/48, kimefanyiwa uhakiki na: Mohammad Abulfadhli Ibrahim, kimesambazwa na: Shirika kuu la vitabu la Kimisri, chapa ya mwaka: 1394H/1974.

kati?﴾ akasema: Ndio nimekuta maeneo manne: Kwenye kauli ya Mola Mtukufu: ﴾**Akasema: Hakika Yeye anasema kwamba ng'ombe huyo si mpevu, wala si kinda, bali ni wa katikati kati ya hao. Basi fanyeni munavyoamrishwa**﴿[1].

Na katika kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴾**Na wale ambao wanapo tumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanakuwa katikati ya hayo**﴿[2].

Na kauli yake Mola Mtukufu: ﴾**Wala usiufanye mkono wako kama ulio fungwa shingoni mwako, wala usiukunjue wote kabisa, utabaki ukilaumiwa muflisi**﴿[3].

Na mwisho kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴾**Wala usitangaze Sala yako kwa sauti kubwa, wala usiifiche kwa sauti ndogo, bali shika njia ya kati na kati ya hizo**﴿[4].

---

(1) Al-Baqarah: 68.
(2) Al-Furqaan: 67.
(3) Al-Israa: 29.
(4) Al-Israa: 110.

7- Tunasisitiza juu ya umuhimu wa utamaduni wa kufikiri katika pande za maisha ya kifikra kisiasa kiuchumi na kiutawala, na kutoka kwenye mzunguko wa chombo kilichokwisha andaliwa na mifumo iliyoganda na kuelekea kwenye mitazamo yenye kufungua fikra na kuifanyisha kazi akili, ni jukumu letu sote kufanya kazi ya kuondoa huu mgando kupitia kufanya kazi ya kueneza utamaduni wa kufikiri kupitia mikusanyiko ya kitamaduni makongamano na vipindi vya mijadala, kwani wapo watu wanazingatia fikra ya kuleta fikra mpya katika Dini ni sawa na kutoka kwenye misingi thabiti na kuibomoa, hata kama jambo la kufanyiwa jitihada halina mahusiano yeyote na misingi hii thabiti, au kwa yale mambo yanayofahamika katika Dini kuwa ni muhimu, na yale yaliyo thibiti moja kwa moja na kuwa na dalili za moja kwa moja, hujengwa mifumo ya mgando wa kifikra – kukufurisha na kuwatoa watu katika Dini – na watu wasio na elimu wala uelewa wa Sharia, si katika watu wanaozingatiwa ni

watu wa kuleta jitihada katika Dini wala watu wenye weledi – au wenye kusoma elimu za Sharia kwenye mifumo yake inayozingatiwa – ni wenye kufanya haraka kuilenga jamii kwa kuzusha mambo kisha kuleta ujinga na kukufurisha watu, mpaka mambo yamefikia hatua ya kulipuka na kuhalalisha umwagaji damu kutokana na Imani zao kali, hali ambayo inahitaji harakati za haraka na za nguvu ili kupambana na mgando huu wa kifikra pamoja na fikra za misimamo mikali iil tuisafishe jamii na ubinadamu kutokana na hatari ya misimamo mikali ya kifikra na yanayofuatana nayo miongoni mwa kufanya vitendo vya kigaidi.

***

## UTAFITI WA NNE.

## MADHUMUNI YA UJUMBE WA UISLAMU NA UMUHIMU WA KUFAHAMU MAKUSUDIO YAKE.

Uislamu wote ni uadilifu, huruma, usamehevu, wepesi na ubinadamu, wasomi wa zamani na wasasa wanasema kila kinachofikia kwenye lengo hili kubwa basi hiko ni katika muundo wa Uislamu, na kinachogongana na hayo hiko kinagongana na Uislamu pamoja na malengo yake na makusudio yake. Uislamu ni Dini ya maadili mema, na Ujumbe wake umekuja kukamilisha maadili haya mema, ambapo Mtume SAW anasema: ﴿Kwa hakika nimeletwa ili kuja kukamilisha maadili mema﴾ [1], ambapo ukweli, utekelezaji wa

(1) Hadithi inayopatikana kwenye kitabu cha Sunani al-kubraa cha Bayhaqy 10/323 Hadithi namba 20782. Dar Al-Kutub Al-Ilmiyah, Beirut nchini Lebanon.

mambo, uaminifu, wema, kuunganisha undugu, ukarimu, usaidizi, murua, kuzuia kero kwa watu, kuondoa maudhi barabarani, kumsaidia mwenye shida, kumsaidia mwenye kutaka msaada, kumu-ondolea matatizo mwenye matatizo vyote hivi ni katika Uislamu sahihi na makusudio yake, amba-po unakuta uongo, usaliti, kukiuka makubaliano, kukata undugu, uovu wa uhasimu, ubinafsi na kuumia moyo kwenye mazuri ya watu, toa mkono wako kwa hawa wenye sifa hizi na kudili nazo, na fahamu kuwa hao watu ni uzito mkubwa kwenye Dini ambayo wao wanajiona wamo kwenye Dini, kwa sababu wao kwa tabia hizi na kwa sifa hizo ni wenye kuwakimbiza watu katika Dini na wala si wenye kuwabashiria mema, ni wenye kupingana na Dini ya kweli na wala si walinganiaji, wakiwa watadhani kinyume na hivyo wakaapa na kufan-ya jitihada basi hakuna kheiri yeyote kwao wala wizani kwenye kiapo chao, ikiwa kauli yao ime-kupendeza na kukushangaza basi kumbuka kauli ya Mwenyezi Mungu Mtukufu: ﴿**Na katika watu yupo yule ambaye maneno yake kwa maisha ya kidunia hukufurahisha; naye humshuhudi-**

**sha Mwenyezi Mungu kwa yaliyomo moyoni mwake, na hali yeye ndiye mkubwa wa uhasimu * Na anapo tawala hufanya juhudi katika nchi kwa kufisidi humo na kuteketeza mimea na viumbe. Na Mwenyezi Mungu hapendi ufisadi * Na akiambiwa: Mwogope Mwenyezi Mungu, hupandwa na mori wa kutenda madhambi. Basi huyo inamtosha Jahannam. Paovu mno hapo kwa mapumziko**}[1].

Na kauli yake Mola Mtukufu: {**Wanapo kujia wanafiki husema: Tunashuhudia ya kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu anajua kuwa wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu anashuhudia ya kuwa hakika wanafiki ni waongo * Wamevifanya viapo vyao ni kinga, na wao wakajizuia kuifuata Njia ya Mwenyezi Mungu. Hakika ni mabaya kabisa waliyo kuwa wakiyafanya * Hayo ni kwa sababu ya kuwa waliamini, kisha wakakufuru; kwa hivyo umepigwa muhuri juu ya nyoyo zao. Kwa hivyo hawafahamu lolote ***

(1) Al-Baqarah: 204 – 206.

**Na unapo waona, miili yao inakupendeza, na wakisema, unasikiliza usemi wao. Lakini wao ni kama magogo yaliyo egemezwa. Wao hudhania kila ukelele unaopigwa ni kwa ajili yao. Hao ni maadui; tahadhari nao. Mwenyezi Mungu awaangamizilie mbali! Vipi wanapotokana haki﴾**[1].

Hakika Uislamu ni Dini ya kazi uzalishaji umakini wa kazi na manufaa kwa watu, ambapo kazi uzalishaji umakini wa kazi na manufaa kwa watu inakuwa ni utekelezaji wa vitendo wa mfumo wa Uislamu, ambapo ukosefu wa ajira uvivu na ujinga wa kwenda sawa na ustaarabu basi toa takbira mara nne kwa yule mwenye kusifika na sifa hizo, hata kama ataitwa kwa majina ya Waislamu na kujihisabu na wao lakini huyo ni mzigo kwenye Dini ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na aibu kwa viumbe wake.

Wasomi wa zamani na wasasa wanasema kuwa malengo na makusudio ya juu ya Sharia katika

(1) Al-Munaafiquun: 1 – 4.

ujumla wake yanazunguka kwenye kufikia masilahi ya waja, ambapo masilahi yanakuwa ndio thamani ya Sharia ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, anasema Imam Abu Ahmad Haamid Al-Ghazaly RA: Tunamaanisha neno masilahi: Ni kulinda makusudio ya Sharia, na makusudio ya Sharia kwa waja ni matano, nayo ni kulinda Dini yao nafsi zao akili zao kizazi chao na mali zao, kila chenye kuingia kwenye kulinda asili hizi tano hicho ndicho kinachozingatiwa ni masilahi, na kila kinchokosekana kwea asili hizi tano basi hicho huzingatiwa ni uharibifu na kuondoa masilahi(1).

Na anasema As-Shatwibiy (2) RA: Kinachofahamika kwenye Sharia ni kuwa imewekwa kwa

---

(1) Kitabu Al-Mustaswfy cha Imamu Ghazaliy ukurasa wa 174, Dar al—Kutubi al-Ilmiyah chapa ya kwanza ya mwaka 1413H sawa na 1993.

(2) Ni Abu Muhammad Abdillah Ibn Ally Ibn Ahmad Ibn Ally Al-Andulus As-Shatwiby, alizaliwa mwaka wa 443H huko Shaatwiby Andulus, na alisoma nchini kwake kwa Ally Aby Abdallah Muhammad Ibn Abi Al-Aas, alifariki mwaka wa 532H, angalia historia yake kwenye kitabu cha Seir Aalaam An-Nablaa 20/92.

ajili ya masilahi ya waja, amri zote ima ni kuondoa uharibifu au kuleta masilahi au vyote viwili kwa pamoja, kinachoingia chini yake kinahukumiwa kwa sababu iliyowekewa, hakuna kwenda kinyume katika hilo kwa kusudio la Sharia, na kilichokatazwa ni kule kukusudia kinyume na makusudio ya Sharia[(1)].

Anasema: Hakika ya Sharia imekuja kwa ajili ya masilahi ya waja, kuamrisha mema na kukataza maovu na kuwa na hiyari vyote hivyo vinarejea kwenye nafasi ya mwenye kupewa jukumu pamoja na masilahi yake, kwa sababu Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mwenye utajiri wa nafasi, mwenye kuepukana na malengo[(2)].

Anasema pia: Sharia zote zinarejea kwenye kulinda masilahi ya waja na kuondoa uharibifu, katika hilo zimeonesha dalili zake jumla na zile maalum, kila mmoja akija na kinyume basi si yenye kuzingatiwa Kisharia[(3)].

(1) Kitabu cha Al-muwaafaqat cha Imamu Shaatwiby 1/318 – Dar Ibn Affaan chapa y a kwanza 1997.
(2) Chanzo kilichopita 1/234.
(3) Chanzo kilichopita 5/230.

Na anasema Ibn Qayyim[1] RA: Hakika ya Sharia jengo lake na msingi wake umesimama juu ya hukumu na masilahi ya waja katika maisha ya duniani na maisha ya akhera, nayo yote ni yenye uadilifu huruma masilahi na hekima, masuala yote yanayokua nje ya uadilifu na kuwa uovu, na kutoka kwenye huruma na kuwa kinyume chake, kutoka kwenye masilahi na kuwa uharibifu, kutoka kwenye hekima na kuwa uovu basi hayo si katika Sharia hata kama kutakuwa kumeingia maelezo mengi, kwani Sharia ni uadilifu wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kati ya waja wake, na huruma yake kati ya waja wake, na ni kivuli chake katika ardhi yake, na hekima zake zenye kumuon-

(1) Ni Izzuddeen Shaikh Al-Islaam Abu Muhammad Ibn Abi Bakri Ibn Ayyub Ibn Saad Ibn Hareez Az-Zarii Msiriya, anafahamika kwa jina la Ibn Qayyimu Al-Juuzyah au Ibn Al-Qayyim, alizaliwa mwaka 691H, ni Mwanachuoni na Mwanajitihada lakini ni mmoja wa Maimamu maarufu wa madhehebu ya Imamu Hambaliy, miongoni mwa vitabu vyake alivyotunga ni pamoja na: Iilaam al-Muwaqqeen, Turuq al-Hukumia fii siasa Shariiyah, alifariki mwaka 751H, soma kitabu iilaam cha Zamarkaly 6/56.

esha Yeye na kuthibitisha ukweli wa Mtume wake SAW[1].

Na anasema Al-Izz Ibn Abdulsalaam [2] RA: Amri zote zinarejea kwenye masilahi ya waja katika dunia yao na akhera yao, na Mwenyezi Mungu Mtukufu ni mwenye utajili kwa waja wote, haumfai utiifu wa wenye utiifu, wala kumdhuru maasi ya wenye kuasi, bali lau wote wangekuwa kwenye uovu wa moyo wa mtu mmoja miongoni mwao basi isingempunguzia chochote kwenye Ufalme wake, na lau wote wangekuwa na ucha-Mungu wa

(1) Kitabu cha Iilaam al-Muwaqqeen cha Ibn Qiyam Al-Juuziyah 3/3.

(2) Ni Izzuddeen Shaikh Al-Islaam Abu Muhammad Abdulaziz Ibn Abdulsalaam, ni Mwanachuoni pekee wakati wa zama zake aliyepachikwa jina la Sultani wa Wanachuoni, alizaliwa mwaka 578H, na alikusanya taaluma mbalimbali ikiwa taaluma ya Tafasiri Hadithi fiqih, na alifikia nafasi ya kuwa mwana jitihada, alifariki mwaka wa 660 H, historia hii inapatikana kwenye kitabu cha Shadharaat Ad-Dhahabu cha Ibn Al-Imaad Al-Hambaly aliyefariki mwaka 1089H 7/522, kimesambazwa na: Dar Ibn Katheer, Damascus – Beirut, chapa ya kwanza mwaka 1406H sawa na 1986.

moyo wa mtu mmoja miongoni mwao basi halitaongeza chochote kwenye Ufalme wa wake, wala hayajafika madhara wakamdhuru wala manufaa yake wakamnufaisha, wote ni wenye kupotea isipokuwa yule aliyeongolewa na Mwenyezi Mungu, na wote ni wenye njaa isipokuwa yule aliyelishwa na Mwenyezi Mungu, na wote wapo uchi isipokuwa yule aliyevishwa na Mwenyezi Mungu[1].

Na anasema: Haijifichi kwa mwenye akili kuwa kupata masilahi na kuondoa uharibifu kwenye nafsi ya mwanadamu na asiyekuwa mwanadamu ni jambo jema na zuri, kutanguliza masilahi bora zaidi ni vyema zaidi na vizuri zaidi, na kuondoa uharibu ulio mbaya zaidi ni vyema zaidi na vizuri zaidi, kutangulizwa masilahi yenye nafasi kubwa zaidi kuliko yale yasiyo na nafsi kubwa ni jambo jema na zuri, na kuondoa uharibifu wenye nafasi kubwa zaidi kuliko masilahi yasiyo na nafasi kub-

(1) Kitabu cha kanuni za hukumu katika masilahi ya waja cha Ibn Muhammad Ezzeddeen Ibn Abdilsalaam 2/23 chapa ya Dar al-Maarif – Beiruti.

wa ni vyema na vizuri zaidi, wamekubaliana wanachuoni juu ya hilo na Sharia pia juu ya uharamu wa kumwaga damu kuharibu heshima ya mtu na mali lakini imehimiza kupata kilichobora zaidi katika kauli na matendo[1].

Ujumla wa mambo ni kuwa: Kufahamu madhumuni ya Uislamu na kujua siri za ujumbe wake wa usamehevu na kusimama kwenye makusudio yake na malengo yake makuu pamoja na kutekeleza hayo yote katika wigo wa mambo mapya ya zama iliyopo na mahitaji yake, inazingatiwa ni jambo muhimu sana katika kupambana na changamoto za zama za sasa, na kupambana na makundi ya kigaidi na misimamo mikali, pamoja na kuzingira fikra za misimamo mikali na kuvunja wigo wa mgando wa fikra na kujifunga kifikra pamoja na uelewa mbaya na peo nyembamba, ili kutoka kwenye hali hii na kuelekea kwenye ulimwengu mpana na wenye wepesi zaidi pia we-

(1) Chanzo kilichopita 1/ 4 .

nye kukomaa na uelewa zaidi wenye muono na kuona lakini pia kufikia masilahi mapana ya nchi na waja na kusambaza misingi mema ya kibinadamu ambayo inaleta usalama na amani pamoja na utulivu na furaha kwa wanadamu wote, hivyo mbora wa watu ni mwenye manufaa zaidi kwa watu, na kinachostahiki kuzaliwa ni kwa mtu mwenye kuishi kwa nafsi yake.

***

## UTAFITI WA TANO.

## MWENENDO WA IBADA NA DESTURI ZA MATENDO.

Miongoni mwa makosa ya wazi kabisa ni kosa la kuchanganya mwenendo wa ibada na desturi za matendo, na kuvesha desturi hizi vazi la mwenendo wa ibada, bali kilicho kibaya zaidi ya hicho ni kujifunga kimawazo na kuendelea na msimamo usio na sababu zinazokubalika kwenye hilo, pamoja na kuwa asili katika Sunna ni kuwa mwenye kuifanya basi ana malipo na thawabu zake na asiyeifanya Sunna anakuwa amepitwa na malipo haya pamoja na thawabu hizi, siku moja aliulizwa Mtume SAW kuhusu Uislamu akasema: ﴿Ni swala tano mchana na usiku﴾ Muulizaji akauliza tena: Je ninapaswa na jambo lengine lisilokuwa swala? Mtume SAW akajibu: ﴿Hapana, isipokuwa kujitolea﴾ Akasema Mtume SAW: ﴿Na funga ya Mwezi wa Ramadhani﴾ Akauliza tena muulizaji: Je ninajukumu lengine lisilo kuwa la kufunga?

Mtume SAW akasema: ﴿Hapana isipokuwa kujitolea﴾ Akasema: Mtume SAW akamtajia yule mtu Ibada ya Zaka, akasema muulizaji: Je napaswa jambo jengine? Mtume SAW akasema: ﴿Hapana, isipokuwa kujitolea﴾ Akazingatia yule mtu huku akisema: Naapa kwa Mwenyezi Mungu sitozidisha kwenye haya wala sitopunguza, akasema Mtume SAW: ﴿Amefaulu akiwa anasema kweli﴾ [1], na akasema Mtume SAW: ﴿Nipeni dhamana ya mambo sita kutoka kwenu, nitawadhamini Pepo, semeni ukweli pindi munapozungumza, tekelezeni ahadi pindi munapo ahidi, tekelezeni amana pindi munapoaminiwa, hifadhini tupu zenu, fumbeni macho yenu na zueni mikono yenu﴾ [2], pindi alipoulizwa Mtume SAW mambo yatakayowaingiza watu wengi peponi, akasema: : "Ni kumcha-Mungu na tabia nzuri"[3].

(1) Hadithi kwenye kitabu cha Sahihi Bukhary – kitabu cha Imani – mlango wa Zaka katika Uislamu, Hadithi ya 56.

(2) Hadithi katika musnad ya Imamu Ahmad 37/ 417 Hadithi namba 22757.

(3) Hadithi ipo katika kitabu cha Sunani ya Imamu Tirmidhy – kitabu cha mambo ya wema na kuunganisha undugu, mlango wa yaliyokuja katka maadili mema, ni Hadithi nambari 2004.

Na majibu yake mengi Mtume SAW juu ya maswali ya wale waliokuwa wanamuuliza kuhusu kuingia Peponi yalikuwa yanazunguka katika utekelezaji wa mambo ya lazima, kujiepusha na madhambi makubwa, shime ya maadili mema, na kila kinachowafaa watu, pindi alipoulizwa Mtume SAW na mtu mmoja amuelekeze matendo yatakayo muingiza Peponi akajibu Mtume SAW kwa kusema: "Kuondoa kero kwenye njia za watu﴿ [1], na anasema tena Mtume SAW ﴾Kuondoa kero njiani ni sadaka"[2], hiyo ni kwa sababu Uislamu umekuja ili kufikia masilahi ya nchi na wananchi kwa maana ya waja na kueneza kila kinachopelekea kufikiwa kwa usalama na amani ya kijamii pamoja na furaha za viumbe wakati huo huo.

---

(1) Kitabu cha Adabu al-mufrad cha Imamu Bukhary ukurasa wa 89 Hadithi namba 228 imefanyiwa uhakiki na: Muhammad Fuad Abdulbaaqy, Dar al-Bashaair al-Islaamiyah – Beiruti

(2) Hadithi inapatikana kwenye Kitabu cha Sahihi Muslimu – Kitabu cha Zaka – mlango wa maelezo kuwa jina la sadaka linakuwa katika aina zote za mambo mema, Hadithi namba 1009

Pamoja na kusisitiza kwetu juu ya shime wa kutekeleza Sunna za Mtume SAW kwa matarajio ya malipo makubwa na thawabu nyingi, tunapaswa kutafautisha kwa uwazi kati ya nini huo mwenendo wa waja na yanayofaungamana na matendo ya desturi, uhimazaji wa Mtume SAW kufunga siku ya Arafah au siku ya Aashuurah ni amri ya kiibada inaingia katika mwenendo wa ibada, vilevile kuanza kwake Mtume SAW kutawadha kwa kuanza kuosha viganja vya kisha kusukutua na kupandisha maji puani pia ni Sunna katika Sunna za ibada, kwa sababu yote hayo ni katika mambo ya ibada, ama yanayoungana na mambo ya mavazi na njia za usafiri na mfano wa hayo, hayo ni katika mlango wa mambo ya desturi na yale yaliyokuwa yanapatikana zama zake Mtume SAW.

Kama vile haiwezekani kwa mwenye akili kusema: Leo sitopanda gari au ndege na nitasafiri kwa kutumia ngamia kama alivyokuwa Mtume SAW akifanya, ni jambo lisilo ingia akilini pia kuse-

ma kuwa nguo hii au ile haikubaliani na Sunna ya Mtume SAW madamu nguo hii inastiri tupu.

Na marejeo ya desturi ni mambo yaliyozoeleka na ya kawaida, pamoja na yale wanayoyaona watu yanakubaliana na zama zao pamoja na mazingira yao na uasilia wa matendo yao, ikiwa tu hayo mambo hayapingani na Sharia thabiti.

Kwa vile tupu ya mwanaume ni kati ya kitovu chake na magoti yake, hivyo kila chenye kustiri hii tupu kisichoonesha wala kushika mwili basi hakuna ubaya wala kupingwa na watu wake ni sawa sawa mtu amevaa kanzu au suti, jambo linalotambuliwa na mazoea na desturi hivyo desturi za watu ni zina hukumu kama ilivyoelezewa na Wanachuoni.

Hakuna ubaya kwa wanachuoni wa dini mavazi yao kuwa ni tofauti na watu wengine, vilevile hali kama hiyo kwa madaktari wanasheria wanajeshi polisi na majaji, lakini kulifanya vazi hili kuwa ni dini na mavazi mengine si katika dini hayo hayajasemwa na mwanachuoni yeyote.

Ni lazima tufahamu, yaliyopokelewa katika rai za baadhi ya wanachuoni katika wigo wa desturi za watu wao na wakati wao pamoja na sehemu zao, ikiwa Imamu Shaafy RA amezingatia kufunika mwanamme kichwa ni katika mambo ya lazima katika murua[1] wa mtu hivyo alichunga hali ya mazingira yake na zama zake, tumeona katika miongo iliyopita na tumeona katika baadhi ya mazingira ya zama za sasa watu wanaozingatia kutovaa kofia kichwani au kufunika kichwa ni mtu aliyekosa murua kwa sababu desturi za watu ni zenye kuvaa kofia au kufunika kichwa kwa mwanaume, ama kulifanya hilo ni dini na alama miongoni mwa alama za wema na ucha-Mungu na mwenye kwenda kinyume na hivyo hutuhumiwa katika dini yake, au kujaribu kuwabebesha watu hilo kwa kuzingatia kwake ni dini au Sunna au maneno ya Kisharia yaliyo lazima kufuatwa, mtazamo huu ni jicho la ujinga na mgando wa kifikra.

(1) Kitabu Al-muwaafaqaat cha Imamu As-Shaatwiby 2/489.

Na yanayo sisitiza kuwa jambo hili linaungana na desturi mazingira na zama ni yaliyosemwa na Imamu As-Shatwiby RA katika kitabu chake na akasema: Ni wazi kichwa cha mwanaume ni kinyume kwa mujibu wa uhalisia, kutofunika kichwa mwanamme ni kwa watu wenye murua ni mbaya katika nchi za Mashariki na si jambo baya kwa watu wa nchi za Magharibi, hukumu ya Kisharia inatofautiana kwa tofauti ya hilo hivyo kwa watu wa Mashariki inasifika ni katika mambo ya uadilifu wakati kwa watu wa Magharibi si lenye sifa hiyo[1].

Hakuna shaka kuwa Imamu As-Shaatwiby RA pia – alichunga hali na mazingira ya zama zake na wala si mazingira ya zama zetu, na yeye amethibitisha hilo ambapo amesema: Hakika asili katika desturi ni kuangalia maana, kwa kusoma tumekuta Sharia inakusudia masilahi ya waja na hukumu za kawaida zinazunguka sawa na zinavyozunguka Sharia, utaona kitu kimoja huzuiliwa katika hali

(1) Chanzo ni kitubu kilichopita 2/520.

isiyokuwa na masilahi, ikiwa ndani yake kuna masilahi basi hufaa[1].

Amepitisha Imamu Al-Quraafy RA: Hakika kupitisha hukumu ambazo zimefahamika na desturi pamoja na kubadilika desturi hizo basi hukumu hizo zinakuwa ni tofauti na makubaliano ya Wanachuoni na ni ujinga katika Dini….bali letu sisi tutatoka ndani ya hiyo nchi na kwenda nchi nyengine, desturi zao zipo tofauti na desturi za nchi ambayo tulikuwa ndani yake basi tukatoa fat'wa kwa mujibu wa desturi za nchi yao pasi ya kuzingatia desturi za nchi ambayo tulikuwa tunaishi, vile vile ikiwa mtu atafika kwetu kutoka nchi desturi zake zipo kinyume na nchi ambayo sisi tunaishi hatutamtolea fat'wa isipokuwa ni kwa kufuata desturi za nchi yake pasi ya kufuata desturi za nchi yetu[2].

Anasema Imamu Ibn Qayyim RA: Mwenye kutoa fat'wa kwa watu kwa kunukuu tu kwenye

(1) Chanzo kilchopita 2/520.
(2) Kitabu Hukumu katika tofauti za Fat'wa cha Imamu Al-Qurafy ukurasa wa 218.

vitabu pasi ya kuangalia tofauti ya mazoea yao desturi zao zama zao sehemu zao hali zao na kulinganisha hali zao basi huyo atakuwa amepotea na kupoteza(1).

Na anasema Ibn Aabideen RA (2): Hakika masuala ya kifiqih ima yawe thabiti kwa tamko la wazi ima yawe thabiti kwa aina ya jitihada na rai, na maswala mengi hujengwa na mwanajitihada sawa na mazoea ya zama zake ambapo lau kutakuwa na tukio katika zama za mazoea ikasemwa tofauti na yaliyosemwa hapo mwanzo, na kwa hili wamesema katika sharti za jitihada: Ni lazima kufahamu desturi za watu, hukumu nyingi hutofautiana kwa tofauti ya zama kwa mabadiliko ya mazoea ya watu wake(3).

---

(1) Kitabu cha Iilaam al-Muwaqqeen cha Ibn Qayyimu 3/16.

(2) Ni Muhammad Ameen Ibn Omar Ibn Abdilaziz Aabideen: Ni Mwanachuoni wa nchi za Shamu ni Imamu wa madhehebu ya Abu Hanifah katika zama zake, miongoni mwa vitabu vyake muhimu alivyotunga ni: Kitabu Raddulmuhtaar, kitabu Rafuu al-Andhaar, kitabu majumuua rasaaili, alifariki mwaka 1252H, angalia kitabu cha Al-Aalaam cha Zarkaly 6/42.

(3) Kitabu cha Rasaaili Ibn Aabideen ﴿Risaalatul uruf﴾ 2/172, Dar al-Kutub al-Ilmiyah.

## UTAFITI WA SITA.

## MATENDO YA MTUME S.A.W KATIKA KUONGOZA NCHI.

Mtume SAW hakuwa ni Mtume tu, bali alikuwa Mtume Nabii kiongozi na kiongozi wa kijeshi, aliyoyafanya kwa kuzingatia ni Nabii na Mtume katika yale yanayofungamana na mambo ya kiimani ibada na maadili mema na ikawa ni sahihi kunasibishwa kwake Mtume SAW yalichukuliwa kwa sura ambayo alibainisha Mtume SAW kwa Maswahaba zake, hakuna tofauti katika kubainisha kwa kutofautiana na zama au sehemu kuwa kwake ni katika mambo yaliyothabiti ni sawa sawa yanakubaliana na mambo ya faradhi kama vile kufunga Ramadhani, Swala, Zaka, Hijja au kufungamana na amri ya Sunna thabiti kutoka kwa Mtume SAW kama vile funga ya Arafah au funga ya Ashura.

Ama aliyofanya Mtume SAW kwa sifa yake kuwa ni Nabii na kiongozi au amefanya kwa sifa yake kuwa ni Nabii na kiongozi wa kijeshi, au kwa sifa yake kuwa Nabii na jaji, basi ufanyaji huo unazingatiwa mara mbili: Kwa kuzingatia Mtume SAW ni Nabii na kwa kuzingatia Mtume SAW ni kiongozi wa kiraia au kiongozi wa kijeshi au kiongozi wa Sharia(1).

Ikiwa jambo la Utume na Ujumbe umeishia kwa kauli ya Mola Mtukufu: ﴿**Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na Mwisho wa Manabii, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu**﴾(2), na amesema Mtume SAW: "Nimefadhilishwa juu ya Mitume kwa mambo sita: Nimepewa jumla ya maneno, nimeshinda vita kwa woga, nimehalalishiwa mali zilizotekwa vitani, nimefanyiwa

(1) Rejea katika hayo: Kitabu cha hukumu katika tofauti ya fat'wa na vitendo vya majaji cha Imamu Al-Qurafy ukurasa wa 99 na kuendelea.
(2) Al-Ahzaab: 40.

ardhi kuwa ni safi na sehemu ya kusujudia, nimepelekwa kwa watu wote, na nimefanywa kuwa ni Mtume wa mwisho"[1], ama aliyoyafanya Mtume SAW kwa kuzingatiwa kuwa ni kiongozi wa wananchi au kiongozi wa kijeshi au jaji matendo hayo yanabakia ni katika masharti na mambo muhimu kufanyika yanayokamilisha sifa nyengine nayo ni kuwa kwa mtumiaji ni kiongozi wa kiraia au kiongozi wa kijeshi au jaji kwa mujibu wa hali, na tunachukuwa ni mfano kwa kila sifa katika sifa hizi.

Aliyoyafanya Mtume SAW kwa kuzingatia ni Mtume na kiongozi wa wananchi ni kauli yake SWA: "Mwenye kuimarisha ardhi iliyokufa basi hiyo ni ardhi yake"[2], anasema Imamu Abu Hanifah RA: ﴿Haya ni kutoka kwake Mtume SAW

(1) Hadithi inapatikana kwenye kitabu cha Sahihi Muslimu – kitabu cha Misikiti na maeneo ya swala, mlango wa nimefanyiwa ardhi kuwa msikiti na safi, ni Hadithi nambari 523.
(2) Hadithi inayopatikana kwenye kitabu cha Sunan Abi Daud – Kitabu cha al-Kharaaj, mlango wa kufufua ardhi iliyokufa ni Hadithi namba 3075.

ameyafanya kama kiongozi – kwa maana kwa sifa yake ya kiongozi – wala haifai kwa yeyote kuifufua ardhi isipokuwa ni kwa ruhusa ya kiongozi, kwa sababu ndani yake kuna umiliki, imefanana na vipande vya ardhi, na vipande vya ardhi vinasimama kwa ruhusa ya Imamu vilevile swala la kufufua ardhi"[1].

Na kwa maelezo hayo, haifai kwa yeyote kuweka mkono wake kwenye kipande cha ardhi na akasema nimeifufua hivyo ni ya kwangu kati yangu na nyinyi ni Hadithi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW, tunasema kumwambia: Hakika Mtume SAW alifanya hivyo kwa sifa ya kiongozi wa wananchi, wala haifai kwa asiyekuwa kiongozi kuchukuwa maamuzi mfano wa haya yanayofungamana na haki ya Umma, au mali ya Umma au miliki ya Umma, kinyume na hivyo basi mambo yatakuwa ni fujo na kufungua milango isiyo-

(1) Kitabu Hukumu katika kutofautisha fat'wa na hukumu pamoja na vitendo vya jaji cha Imamu Al-Qurafy ukurasa wa 111.

fungika ya fitina na uadui katika miliki ya Umma, huenda ikaleta vita na mauaji kati ya watu, lakini ni lazima kuwajibika katika hilo kufuata Katiba na sheria ambazo zinasimamia mambo ya nchi na wananchi.

Katika yale aliyoyafanya Mtume SAW kwa kuzingatiwa ni kiongozi wa kijeshi ni kauli yake SAW: "Mwenye kuuwa mtu akawa na ushahidi wa hilo basi anayohaki ya kuchukua ngawira za aliyeuwawa"[(1)], haifai kwa yeyote hivi sasa kufanya hivyo, ikiwa ameua gaidi katika kupambana naye basi haifai kwake kusema: Mimi ni bora kuliko silaha yake au gari yake au simu yake au mali zake, kwa sababu kufanya kwa Mtume SAW kulikuwa ni kwa sifa yake kiogozi wa kijeshi, lakini kilicho lazima katika hilo ni mfumo wa sheria na Katiba za sasa pamoja na mfumo wa nchi na majeshi yake.

(1) Hadithi inayopatikana kwenye kitabu cha Sahihi Bukhary – Kitabu cha ulazima wa kutoa sehemu ya tano, mlango wa mtu asiye toa sehemu ya tano, ni Hadithi namba 3142.

Aliyoyafanya Mtume SAW kwa kuzingatiwa ni jaji ni kauli yake SAW katika kadhia ya kujivua kwenye ndoa ambapo alikuja mke wa Thabiti Ibn Qais kwa Mtume SAW na akasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu, Thabit Ibn Qais si hitaji kuachana naye kwa sababu ya tabia zake wala mapungufu kwenye dini yake, lakini mimi nachukia ukafiri ndani ya Uislamu, akasema Mtume SAW: "Je unataka bustani yake", akasema: Ndio, akasema Mtume SAW: "Pokea bustani na mwache moja kwa moja"[1], Mtume alifanya hivyo kwa kuzingatia ni Nabii na jaji, nayo pia ni katika mambo ambayo huandaliwa na sheria ndani ya zama zetu ni lazima kuwajibika nayo sawa na yalivyoandaliwa na sheria, nayo hufahamika kwenye Fiqihi ya Kiislamu kama kupata talaka kwa kadhi, ambako kuna vigezo vyake vya Kisharia na kisheria.

***

(1) Hadithi inapatika kwenye kitabu cha Sahihi Bukhary – Kitabu cha talaka, mlango wa kujivua kwenye ndoa na namna gani hutoka talaka, ni Hadithi nambari 4990.

## UTAFITI WA SABA.

## MIFANO YA KIUTENDAJI YA UFAHAMU UNAOKUSUDIWA WA SUNNA ZA MTUME

### Mfano wa Kwanza
### Ufahamu wa Hadithi za Mswaki

Kutoka kwa Abi Huraira RA hakika ya Mtume SAW amesema: "Lau nisingewaonea huruma watu wa Umma wangu basi ninge waamrisha kupiga mswaki katika kila swala"(1).

Kutoka kwa Zaid Ibn Khalid Al-Juhniy RA amesema: Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW anasema: "Lau nisingeona uzito kwa Umma wangu basi ningewaamrisha kupiga mswaki kila wakati wa swala"(2).

(1) Sahihi Bukhary – Kitabu cha Ijumaa, mlango wa mswaki siku ya Ijumaa ni Hadithi namba 887.
(2) Sunani ya Abi Daud – Kitabu cha mambo ya usafi, mlango

Kutoka kwa Abi Hurairah RA toka kwa Mtume SAW amesema: "Lau nisingeona uzito kwa Umma wangu basi ningewaarimsha kupiga mswaki kila wanapo tawadha"(1).

Kutoka kwa Hudhaifah RA amesema: Alikuwa Mtume SAW "Pindi anaposimama usiku anasugua mdomo wake kwa mswaki"(2).

Kutoka kwa Al-Miqdam Ibn Shuraih, kutoka kwa baba yake RA amesema: Nilimuuliza Bibi Aisha RA, ni kasema: Ni kitu gani alikuwa Mtume SAW anaanza nacho pindi anapoingia nyumbani kwake? Akajibu: ﴿Alikuwa anaanza na mswaki"(3).

---

wa upigaji mswaki, ni Hadithi nambari 46, na Sunani ya Ibn Maja – Kitabu cha mambo ya usafi na utwahara pamoja na suna zake, mlango wa mambo ya upigaji mswaki, Hadithi ya 287 chapa ya Dar Ar-risaalah al- Aalamiyah.

(1) Hadithi imo kwenye Sunani ya Aby Duad – Kwenye maudhui iliyopita.

(2) Sahihi ya Imamu Bukhary – Kitabu cha mambo ya udhu, mlango wa matumizi ya mswaki, ni Hadithi namba 245, na kwenye kitabu cha Sahihi ya Imamu Muslimu – Kitabu cha mambo ya usafi, mlango wa matumizi ya mswaki, Hadithi namba 255.

(3) Sahihi ya Imamu Muslimu – Kitabu cha mambo ya usafi na utwahara, mlango wa matumizi ya mswaki. Hadithi nambari 253.

Kutoka kwa Aamir Ibn Rabeea amesema: "Nilimuona Mtume SAW anapiga mswaki hali ya kuwa amefunga"(1).

Mtume SAW amebainisha hekima ya matumizi ya mswaki na kudumu katika kutumia ambapo amesema: "Mswaki ni wenye kusafisha mdomo na wenye kuridhiwa na Mola"(2).

Ikiwa makusudio ya matumizi ya mswaki ni kusafisha mdomo na kulinda afya yake, pamoja na kuleta harufu nzuri ya mdomo, kuondoa athari zozote za harufu yeyote yenye kuchukiza ikiwa ni pamoja na kulinda meno na ufidhi kuupa nguvu, basi makusudio haya kama yanavyofikiwa kwa kutumia mti wa mswaki unaochukuliwa kutoka kwenye mti wa mswaki basi pia hufikiwa kila kinachofikiwa na lengo hili, hakuna ubaya kufanya hivyo kwa kutumia mti wa mswaki au usiokuwa mswaki wa mti, kama vile kutumia dawa ya meno

(1) Ni Hadithi inayopatikana kwenye Sahihi ya Imamu Bukhary – Kitabu cha mambo ya funga, mlango wa matumizi ya mswaki mbichi na mkavu kwa mwenye kufunga.
(2) Chanzo kilichopita, kwenye maudhui hiyo hiyo.

pamoja na mswaki wa brush na mifano ya hivyo, ama kushikamana na uwazi wa tamko na kuhukumu jambo moja kwa moja na kuhusisha moja kwa moja mswaki wa mti na mwengine wowote, na kuupendezesha mti huu wa mswaki kuwa ni katika alama za ucha-Mungu na wema, kwa kuuweka huu mswaki wa mti au miswaki miwili au mitatu kwenye mfuko mdogo wa juu ya shati au kanzu, pamoja na uwezekano wa kupatwa na vumbi pamoja na athari zengine za hali ya hewa, na tunadhania kuwa sisi kwa kufanya hivyo tu pasi ya vyengine basi tunaifikia Sunna yenyewe, na mwenye kufanya tofauti na hivyo tuna muona si mwenye kufuata Sunna, hii ni aina ya mgando wa kifikra na peo nyembamba kwa mwenye kuganda kwenye uwazi wa tamko la Hadithi pasi ya kufahamu umbali wake malengo yake na makusudio yake, kwani Mtume SAW pamoja na Maswahaba zake walitumia kile kilichokuwa chepesi wakati wa zama zao, lau wangeishi kwenye zama zetu hizi basi wangetumia kilicho bora zaidi na manufaa na kipya katika vilivyofikiwa na tafiti za kielimu kwenye mambo mbalimbali.

## MFANO WA PILI.

## UELEWA WA HADITHI ZA USAFI WA KITANDA.

Kutoka kwa Abi Hurairah RA hakika ya Mtume SAW amesema: "Mmoja wenu anapokwenda kulala kwenye kitanda chake basi na achukue kitambaa chake na akung'utie kitanda chake, na amtaje Mwenyezi Mungu, kwa sababu hawezi kujua kilichopo nyuma yake baada ya hapo kwenye kitanda chake, pindi anapotaka kulalia ubavu basi na alalie ubavu wake wa kulia, na asema: Utakasifu ni wako Ewe Mola wangu kwako nimeuweka ubavu wangu, na kwako ninauinua, ikiwa utaichukua nafsi yangu basi naomba uisamehe, ikiwa utaiamsha basi naomba uilinde kwa kile unachowalindia waja wako wema"(1).

(1) Hadithi inapatikana kwenye kitabu cha Sahihi Bukhary – Kitabu cha maombi, mlango wa kujilinda na sheitani wakati wa kulala, Hadithi namba 6320, na imepokelewa kwenye

Na kutoka kwa Abi Hurairah RA hakika ya Mtume SAW amesema: "Pindi mmoja wenu anaposimama kutoka kwenye kitanda chake kisha akarudi tena kwenye kitanda chake basi na akung'ute kwa ncha ya kitambaa chake mara tatu, kwa sababu hawezi fahamu kitakachotokea nyuma yake hapo baadaye, pindi anapolalia ubavu basi na aseme: Kwa jina lako Mola wangu nimeuweka ubavu wangu, na kwako ninauinua, ikiwa utaifisha nafsi yangu basi naomba uisamehe, na ikiwa utaiamsha basi ihifadhi kwa kile unachowahifadhia waja wako wema, pindi akiamka na aseme: Shukrani ni za Mwenyezi Mugu ambaye ameponya mwili wangu na akanirudishia roho yangu na kuniamrisha kumtaja Yeye"[1].

---

kitabu cha Sahihi Muslimu – Kitabu cha maombi toba na kuomba msamaha, mlango wa anayoyasema wakati wa kulala na kuwa kitandani, Hadithi namba 2714.

(1) Hadithi ipo kwenye kitabu cha Sahihi Bukhary – Kitabu cha Taweed, mlango wa kuomba kwa kutumia majina ya Mwenyezi Mungu Mtukufu na kujilinda na sheitani kwa majina hayo, ni Hadithi namba 7393, na imepokelewa na Sunani Tirmidhy mlango ya maombi kutoka kwa Mtume SAW. Hadithi namba 3401.

Kutoka kwa Abi Hurairah RA amesema: "Pindi mmoja wenu anaposimama usiku kutoka kwenye kitanda chake, kisha akakirudia hawezi fahamu yaliyo nyuma hapo baadaye basi na akung'ute kitanda chake kwa kitambaa chake au sehemu ya kitambaa chake, pindi akilalia ubavu basi na aseme, kwa jina lako nimeweka ubavu wangu na kwako ninauinua ikiwa utaifisha nafsi yangu basi naomba isamehe, ikiwa utaiamsha basi naomba uilinde kwa kile unachowalindia waja wako wema"[1]. Ni Sunna kwa mtu kukung'uta kitanda chake kabla ya kukilalia kwa kutumia nchi ya nguo yake ili asijepatwa mkononi mwake na kitu kinachochukiza.

Ikiwa tutasimama kwenye uwazi wa tamko au andiko basi mtu anayevaa nguo ambayo inakuwa ngumu kwake kushika ncha yake na kuondoa

(1) Musnad Al-Bazzaar 15/161 Hadithi namba 8506, imefanyiwa uhakiki na: Mahfoudh Rahman Zeynuddeen, usambazaji ni Maktaba ya Sayansi na Kanuni – Madinah, chapa ya kwanza 1988.

kero kwenye sehemu anayolalia atafanya nini!! Kama vile mtu kuvaa nguo za kisas zisizowezekana kufanya hivyo.

Lau tutaangalia makusudio makuu nayo ni kusafisha sehemu ya kulala na kuhakikisha hakuna kitu kinachoweza kumsababishia binadamu kero ya aina yeyote ikiwa kama wadudu wadogo wadogo na mfano wake, tutafahamu kuwa binadamu anaweza kufanya hivyo kwa kutumia chombo chochote cha kisasa kinachofanikisha makusudio kama vile kutumia kitu cha kukung'utia au fagio au mfano wa hivyo, zingatio sio kushika ncha ya nguo bali ni kile kinachofanikisha kufikiwa kwa usafi wa sehemu na kuhakikisha sehemu ipo salama kutokana na kile kinachowezekana kusababisha kero kwa binadamu, bali katika hilo hufikiwa kwa kukung'uta au mfano wake zaidi ya yale yanayofikiwa kwa kutumia ncha ya nguo, lakini Mtume SAW aliuambia Umma wake kwa kile kilicho kwenye kawaida yao na chenye wepesi kupatikana ndani ya zama zao ili kusiwe na uzito kwao katika wigo wa waliyo nayo kwenye maisha

yao duni, kana kwamba Mtume SAW anawaambia: Safisheni sehemu zenu za kulala kabla ya kwenda kulala kwa kutumia kitu kilichokuwa chepesi kwenu kukipata hata kwa kutumia ncha za nguo zenu.

Wakatoa sababu baadhi ya washereheshaji wa Hadithi maelekezo ya kuchukua ncha ya nguo ni kuwa Mtume SAW ameelekeza hivyo ili mkono usipate kero ya kutumia chombo chenye makali au kutumia ncha ya kibao cha ubapa, au kupatwa na vumbi au kugongwa na nyoka au nge au mfano wake katika vyenye kuleta kero na maumivu, au kutumia fimbo ndogo inamletea kero mwenye kulala hali ya kuwa haisi kitu, au mfano wa hayo ikiwa mwanadamu atakusudia kufanya usafi wa sehemu yake ya kulalia kwa mkono wake [(1)], inasisitiza maana ambayo tumeielezea.

(1) Angalia sherehe ya nawawi ya Sahihi Muslimu 17/37 kinasambazwa na Dar Akhbaar Turaath al-Araby – Beirut, na kitabu cha Tuhfah al-Ahwadhy sherehe ya Jaamii Tirmidhy 9/244 kinasambazwa: Dar al-Kutub al-ilmiya, Beirut, na kitabu cha al-Ifswaah aan Maany as-Swahhah cha Ibn Hubeirah 281 chapa ya Dar al-Watwan.

Pamoja na hayo mwenye kufananisha maisha yake na maisha yao hakuna makosa kwake ikiwa atachukuwa na kufanyia kazi uwazi wa Hadithi na kusafisha sehemu yake ya kulala kwa kutumia ncha ya nguo yake, sio kujaribu kuwabebesha watu wote kuchukuwa maana ya wazi ya Hadithi pasi na vyengine inazingatiwa ni kubana mambo katika ufahamu wao wa makusudio ya Hadithi na kuwafanyia watu uzito katika mambo yao ya maisha.

Kama vile kuzingatia kwa mwenye kutaka kuwabebesha watu uwazi wa andiko kuwa ufahamu wake pekee ni ufahamu unaokubaliana na Sunna ya Mtume SAW na isiyokuwa hiyo haikubaliani na Sunna – Pamoja na maendeleo ya maisha yetu ya sasa – hiyo ni dhuluma ya wazi kwenye Sunna za Mtume SAW, na ni uelewa wenye makosa usiokubaliana na makusudio makuu ya Sharia ikiwa ni pamoja na kuwa na shime ya kiwango cha juu ya usafi na uzuri pamoja na kuchukuwa njia zote za

kimaendeleo na ustawi, madamu ni katika wigo halali ambao hakuna uharamu ndani yake, ikiwa ni kwenda sawa na kanuni kuwa asili ya mambo ni halali pindipo hakuna andiko la uharamu, kutoka kwa Abi Thaalabah Al-Khushany RA amesema: Amesema Mtume SAW: "Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amelazimisha mambo basi musiyapoteze, akaharamisha vilivyo haramu wala musivikiuke, akaweka mipaka wala musiivuke, akanyamazia baadhi ya mambo pasi ya kusahau wala musiyatafute mambo hayo"(1), kutoka kwa Ibn Abbas RA amesema: Watu wa zama za ujinga walikuwa wanakula vitu na wanaacha vitu kwa uchafu, Mwenyezi Mungu akamleta Mtume wake SAW na kuteremsha Kitabu chake, akahalalisha halali yake na kuharamisha haramu yake, alichohalalisha hicho ni halali na alichoharamisha hicho

(1) Sunan Daar Al-Qutwuny – Kitabu cha mambo ya unyonyeshaji 5/325. Hadithi namba 4396 chapa ya Taasisi ya Risaalah Beirut – Lebanon.

ni haramu, na alichokinyamazia basi hiko kimesamehewa, akasoma Aya hii: ﴿**Sema: Sioni katika yale niliyo funuliwa mimi kitu kilicho haramishwa kwa mlaji**﴾[1].

****

(1) Imepokelewa na Hakim katika musnadi yake 4/128 Hadithi namba 7113.

## MFANO WA TATU

## UFAHAMU WA HADITHI YA KUREFUSHA NGUO.

Kutoka kwa Ibn Omar RA: Mtume SAW amesema: "Mwenyezi Mungu hamuangalii mwenye kurefusha nguo yake kwa kiburi"(1).

Kutoka kwa Abdillah Ibn Umar RA anasema: Amesema Mtume SAW: "Mwenye kurefusha nguo yake kwa kiburi Mwenyezi Mungu hatomuangalia siku ya Kiyama﴾ nikamuuliza Muharib: Ametaja

(1) Hadithi imo kwenye kitabu cha Sahihi Bukhary – Kitabu cha mambo ya mavazi, mlango wa kauli ya Mwenyezi Mungu {Sema: Sioni katika yale niliyo funuliwa mimi kitu kilicho haramishwa kwa mlaji﴾Hadithi namba 5783, na kitabu cha Sahihi Muslimu – Kitabu cha mambo ya mavazi na mapambo, mlango wa uharamu wa kurefusha nguo kwa kiburi, Hadithi namba 2085.

kitambaa chake? Akasema: Hakuhusisha kitambaa wala kanzu"[1].

Kutoka kwa Abdillah Ibn Umar RA amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW: "Mwenye kurefusha nguo yake kwa kiburi, Mwenyezi Mungu hatomuangalia siku ya Kiyama﴾ akasema Abubakr: Upande mmoja wa nguo yangu unapwaya kwenda chini ispokuwa huwa ninauinua upande huo, Mtume SAW akasema: Hakika wewe si mwenye kufanya hivyo kwa kiburi﴾ Musa akasema: Nilimuuliza Saalim je Abdallah alitaja mwenye kurefusha kilemba chake? Akasema: Sikumsikia isipokuwa ametaja nguo yake"[2].

Kutoka kwa Ibn Omar RA kuwa alimuona mtu akirefusha nguo yake, akasema: Ni nani wewe?

(1) Hadithi ipo kwenye Sahihi Bukhary – kitabu cha mavazi, mlango wa mwenye kurefusha nguo yake kwa kiburi, Hadithi namba5791.
(2) Hadithi imo kwenye Sahihi Bukhary – Kitabu kinachozungumzia ubora wa Maswahaba wa Mtume SAW, mlango wa kauli ya Mtume SAW: Lau ningemfanya rafiki. Hadithi namba 3665.

Akajinasibisha na yeye, tahamaki yule mtu ni kutoka kabila la Baniy Laith, Ibn Omar akamfahamu, akasema: Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW kwa masikio yangu haya mawili anasema: "Mwenye kurefusha nguo yake akakusudia kufanya hivyo kwa kuonesha kiburi, basi Mwenyezi Mungu hato muhurumia huyo mtu siku ya Kiyama"[(1)].

Kutoka kwa Abi Dharr RA kutoka kwa Mtume SAW amesema: "Watu wa aina tatu Mwenyezi Mungu hatowazungumzisha siku ya Kiyama, wala kuwaonea huruma wala kuwatakasa na wana adhabu kali, anasema: Mtume SAW ameyasema maneno hayo kwenye Hadithi tatu, akasema Abu Dharri: Wamedhalilika na wamepata hasara, ni wakina nani hao Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu? Akasema: Mwenye kurefusha nguo, Mwenye

(1) Hadithi ipo kwenye Sahihi Muslimu – Kitabu cha mambo ya mavazi na mapambo, mlango wa uharamu wa kurefusha nguo kwa kiburi, na maelezo ya kinachofaa kurefusha na kile kilichokuwa ni sunna, Hadithi namba 2085.

kutajataja neema alizompa nduguye na mwenye kutangaza bidhaa zake kwa kiapo cha uongo"[1].

Kutoka kwa Abi Hurairah RA toka kwa Mtume SAW amesema: "Nguo iliyofikia chini ya vifundo viwili vya miguu basi huyo ni mtu wa motoni"[2].

Kwa kuangalia Hadithi zilizotajwa tunasisitiza kuwa sababu ambayo inajengewa kwenye katazo la kurefusha nguo ni kile kiburi, ambacho kina maanisha kujitukuza na kujiinua na kuleta kiburi kwa waja wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ikiwa ni

---

(1) Hadithi ipo kwenye kitabu cha Sahihi Muslimu – Kitabu cha mambo ya Imani, mlango wa unaoelezea uharamu wa kurefusha nguo, kutajataja kilichotolewa, kutangaza bidhaa kwa kiapo cha uongo, na maelezo ya watu wa aina tatu ambao Mwenyezi Mungu hatowazungumzisha siku ya Kiyama, wala kuwaonea huruma, wala kuwatakasa na wana adhabu kali. Hadithi namba 106.

(2) Hadithi inapatikana kwenye kitabu cha Sahihi ya Imamu Bukhary – Kitabu cha mambo ya mavazi, mlango wa nguo inayofika chini ya vifundo viwili huyo ni mtu wa motoni, Hadithi namba 5787, na inapatikana kwenye kitabu cha Sunani An-Nisaa- Kitabu cha mapambo, mlango wa nguo iliyofikia chini ya vifundo viwili. Hadithi namba 5331.

kujiona na kujifaharisha kwa nguo ndefu ambayo wakati huo ilikuwa inazingatiwa ni mandhari katika mandhari za kuwa na nafasi, bali mapokezi ni kuwa ﴿Hayakusudii hivyo isipokuwa kwa mwenye kufanya kiburi﴾ katazo limehusika kwenye kuleta kiburi, wakati wowote kunapokuwa na hali ya kiburi ndipo kuna katazo na uharamu, na wakati wowote inapoondoka hali ya kiburi sababu ya katazo na uharamu navyo huondoka, imetajwa sababu hii kwa uwazi kabisa kwenye Hadithi ya: Kwanza ya Pili ya Tatu na ya Nne.

Ama Hadithi "Nguo inayofika chini ya vifundo viwili vya miguu huyo ni mtu wa motoni", na Hadithi iliyomtaja mwenye kurefusha nguo katika watu wa aina tatu ambao Mwenyezi Mungu hatowazungumzisha wala kuwaonea haruma siku ya Kiyama, kila mmoja kati yao kuna Hadithi ya moja kwa moja, pindi inapokutana Hadithi ya moja kwa moja pamoja na ile yenye vigezo basi hufanyiwa kazi ya moja kwa moja, madamu vigezo vimekuja katika Hadithi zengine ni msisiti-

zo kuwa katazo la kurefusha nguo linafungamana na hali ya kiburi hii ndio imekuwa sababu kuu ya kukataza na kupata dhambi na sio kwa sababu tu ya nguo kuwa ndefu.

Ametaja Imamu An-Nawawy [(1)] RA: Ama kigezo cha kiburi kinahusisha ujumla wa warefushaji wa nguo, na dalili ya kuwa kusudio la adhabu kali kwa mwenye kurefusha nguo kwa kiburi, ni kuwa Mtume SAW ameruhusu katika hilo kwa Abi Bakri Swadiq RA na akasema kumwambia: Wewe si katika hao Ewe Ababakri ambapo urefushaji wake haukuwa kwa lengo la kuleta kiburi [(2)].

Akasema Ibn Hajar [(3)] RA: Amechukulia dalili

(1) Naye ni Abu Zakaria Yahyaddeen, Yahya Ibn Sharafu An-Nawawiy As-Shaafy, anatokea kijiji cha Hauraan nchini Syria, alizaliwa mwaka wa 631H, ni alama ya Fiqhi na Hadithi, katika jumla ya vitabu vyake ni pamoja na: Al-Minhaaj katika sherehe ya kitabu cha Sahihi Muslim, na kitabu cha Riyadh Swaaliheen, alifariki mwaka wa 676H, soma kitabu cha Al-Iilaam cha Zarkary 8/149.

(2) Sherehe An-Nawawy ya kitabu cha Sahihi Muslimu 2/116.

(3) Ni Sheikh Al-Islaam Abufadhli Shihabudeen Ahmad Ibn Ally Ibn Muhammad Al-Asqalaany, anayefahamika kwa jina la Ibn Hajar, alizaliwa mwaka wa 773H, miongoni mwa utunzi wake ni pamoja na kitabu cha Fat'hulbaary, Lisaanul Miizaan, alifariki mwaka 852H. Kitabu cha Iilaam cha Zarkaly 1/178.

kigezo kwenye Hadithi hizi kwa hali ya kiburi kuwa kukataza moja kwa moja kulikokuja kwenye kukataza kurefusha nguo inachukuliwa kwa mwenye kufanyiwa kigezo, kwani hakuna uharamu kurefusha nguo ikiwa amesalimika na hali ya kiburi [1].

Amesema Al-Haafidh Al-Iraaqy [2] RA: Ama Hadithi za moja kwa moja kuwa nguo iliyofika chini ya vifundo viwili vya miguu huyo ni mtu wa motoni, kusudio ni kwa yule aliyekuwa na lengo la kufanya kiburi, kwa sababu Hadithi ya moja kwa moja hivyo ni lazima kumbebesha mwenye kuwekewa kigezo [3].

(1) Kitabu Fat'hulbaary sherehe ya Sahihi Bukhary cha Ibn Hajar al-Asqalaany 10/263 nimetolewa na Dar: Al-Maarifah – Beirut.
(2) Ni Abufadhli, Zeynudeen Abdulraheem Ibn Al-Hussein Ibn Abdulrahman, anafahamika kwa jina la Al-Haafidh Al-Iraaqy, miongoni mwa wahifadhi wakubwa wa Hadithi, aiizaliwa mwaka wa 725H. Miongoni mwa vitabu vyake ni pamoja na kitabu cha Al-Mughny na Al-Ulfiya, alifariki mwaka wa 806H. Kitabu cha Iilaam cha Zarkaly 3/344.
(3) Kitabu cha Twarhe At-Tasharrub katika sherehe ya At-Taqreeb cha Zeynudeen Al-Iraaqy 8/174, chapa ya Kimisri ya zamani.

Amesema Shaukany RA: Ni lazima kubebesha kauli yake "Ni kwa mwenye kufanya kiburi» katika Hadithi ya Jabir kuwa imetoka kwenye matoko ya kawaida, inakuwa adhabu iliyotajwa katika Hadithi ni yenye kuelekea kwa mwenye kufanya hivyo kwa sababu za kiburi, na kauli kuwa kurefusha nguo ni katika hali ya kuonesha kiburi ni kufanyia kazi uwazi wa Hadithi ya Jabir imekuja iliyopokea kwa dharura, na kuja kauli yake Mtume SAW kwa Abibakri: «Hakika yako si miongoni mwa wanaofanya hivyo kwa kiburi"[1].

Imepokelewa kuwa Aba Hanifah [2] R.A alivaa kitambaa chenye thamani kubwa gharama yake ni kiasi cha Dinal mia nne, na alikuwa akiiburuza ardhini akaulizwa: Je hatukuwa ni wenye kukataz-

(1) Kitabu cha Nail Al-Utwaar cha Shaukany 2/133 kimetolewa na Dar: Al-Hadithi Misri.

(2) Ni Imamu Abu Hanifah An-Nuumaan Ibn Thaabit Al-Kuufy, ni mwanasharia na mwanachuoni wa Kiiraqi, ni mmoja wa Maimamu wanne wa watu wa Sunna, ndio mwenye madhehebu maarufu, alizaliwa mwaka wa 80H na alifariki mwaka 150H. Kitabu cha Seir Iilaam An-Nablaa 6/390.

wa na hili? Akajibu: Limekatazwa hilo kwa watu we-nye kufanya kiburi na sisi hatukuwa miongoni mwao [1].

Kwa vile sisi tumesisitiza na bado tunaendelea kusisitiza kuwa jambo la kuvaa ni katika upande wa mambo ya tamaduni na wala sio mambo ya ibada, sababu ya kukatazwa inajengeka kwenye hali ya kiburi, wakati wowote itakapo kuwepo hali hiyo basi katazo linakuwa ni lenye nafasi, na wakati wowote inapoondoka sababu basi katazo nalo linaondoka, pamoja na msisitizo wetu juu ya umuhimu wa kuchunga yanayopelekea kukubalika na jamii nzima pamoja na kulinda usafi wa nguo kwa kurefuka kwake isibebe uchafu na mfano wake.

***

(1) Kitabu cha Al-Adabu Sharia cha Ibn Maqlah Al-Maqdasy 3/521, kinasambazwa na: Aalamu al-Kutub.

## MFANO WA NNE.

## UELEWA WA HADITHI ZA SADAKA YA FITRI.

Kutoka kwa Ibn Omar RA amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW amelazimisha Zaka ya Fitri pishi moja ya tende au pishi moja ya ngano nzima kwa mtumwa, mtu huru, mwanaume, mwanamke, mdogo na mkubwa katika Waislamu, na akaamrisha kulipwa Zaka hiyo kabla ya watu kutoka kwenda kuswali"(1).

Kutoka kwa Abi Said RA amesema: "Tulikuwa tunatoa Zaka ya Fitri pishi moja ya chakula au pishi moja ya ngano nzima au pishi moja ya tende au pishi mbili za zabibu"(2).

---

(1) Hadithi ipo kwenye Sahihi Bukhary – Kitabu cha Zaka, mlango wa ulazima wa Zaka ya Fitri, Hadithi namba 1503, na inapatikana kwenye Sahihi Muslimu – Kitabu cha Zaka ya Fitri kwa Muislamu kutokana na tende na ngano nzima, Hadithi namba 984.

(2) Hadithi ipo kwenye Sahihi Bukhary – Kitabu cha Zaka, mlan-

Kutoka kwa Amru Ibn Shuaib kutoka kwa baba yake kutoka kwa babu yake: "Hakika Mtume SAW alituma mlinganiaji katika maeneo ya mji wa Makkah: Fahamu hakika Zaka ya Fitri ni lazima kwa kila Muislamu mwanaume au mwanamke huru au mtumwa mdogo au mkubwa, vibaba viwili vya ngano ya unga au isiyokuwa hiyo pishi moja ya chakula"[(1)].

Kutoka kwa Ibn Abbas RA amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu amelazimisha Zaka ya Fitri ili kumsafisha na kumtakasa mfungaji kutokana na vitendo vya kipuuzi na maneno machafu, na ni chakula kwa watu masikini, basi mwenye kuitekeleza kabla ya Swala ya Eid hiyo ni Zaka yenye kukubaliwa, na mwenye kuitekeleza baada

---

go wa ulazima wa Zaka ya Fitri pishi moja ya chakula, Hadithi namba 1506. Ipo kwenye kitabu cha Sahihi Muslimu – Kitabu cha Zaka, mlango wa Zaka ya Fitri kwa Waislammu inayotokana na tende na ngano. Haditi namba 985.

(1) Hadithi ipo katika Sunani Tirmidhy – Kitabu cha Zaka, mlango wa yaliyokuja katika Zaka ya Fitri. Hadithi namba 674.

ya Swala ya Eid hiyo ni sadaka miongoni mwa sadaka"[1].

Kutoka kwa Naafii, kutoka kwa Ibn Omar RA amesema: "Mtume SAW amelazimisha Zaka ya Fitri – au amesema: Zaka ya Ramadhani – kwa mwanaume, mwanammke, mtu huru, mtumwa, pishi moja ya tende, au pishi moja ya ngano nzima, watu wakafanya usawa wa nusu pishi ya ngano ya unga. Ibn Omar RA alikuwa anatoa tende, wakazi wa Madinah wakakosa akatoa ngano nzima, Ibn Omar alikuwa akiwapa watoto wadogo watu wakubwa hata ikiwa wa kupewa ni katika watoto wanaotokana na yeye, na Ibn Omar alikuwa akiwapa wale wanayoikubali hiyo Zaka na walikuwa wakiitoa siku moja kabla ya siku ya Fitri ka siku moja au siku mbili [2].

---

(1) Sunani Abi Daud – Kitabu cha Zaka, mlango wa Zaka ya Fitri. Hadithi namba 1609, na ipo kwenye Sunani ya Ibn Majah – kwenye milango ya Zaka, mlango wa Zaka ya Fitri. Hadithi namba 1827.

(2) Inaptikana kwenye Sahihi Bukhary – Kitabu cha Zaka, mlango wa Zaka ya Fitri kwa mtu huru na mtumwa. Hadithi namba 1511.

Kutoka kwa Abi Said Al-Khudry RA amesema: Tulikuwa tunaitoa wakati wa Mtume SAW pishi moja ya chakula, au pishi moja ya tende, au pishi moja ya ngano nzima, au pishi ya zabibu, alipokuja Muawiyah akaja na chakula cha ngano kavu, akasema: Ninaona kibaba kimoja cha hizi ni sawa na vibaba viwili [(1)].

Katika mapokezi ya Muslimu kutoka kwa Abi Saidi RA amesema: "Tulikuwa tukitoa wakati wa Mtume SAW Zaka ya Fitri, kwa kila mtoto mdogo, mtu mkubwa, mtu huru, mtumwa pishi moja ya chakula, au pishi moja ngano nzima, au pishi ya tende, au pishi ya zabibu, hatukuacha kutoa nafaka hizo mpaka alipokuja Muawiya Ibn Abi Sufyan kwenye Hija au kwenye Umra na akazungumza na watu kwenye mimbari, aliyokuwa ameyazungumza ni pamoja na kusema: Hakika yangu mimi ninaona kuwa vibaba viwili vya ngano ya shamu

---

(1) Hadithi inapatikana kwenye kitabu cha Sahihi Bukhary – Kitabu cha Zaka, mlango wa pishi ya zabibu. Hadithi namba 1508.

ni sawa sawa na pishi moja ya tende, ndipo watu wakachukua hivyo"[1].

*Katika tamko lengine: "Tulikuwa tunatoa Zaka ya Fitri na Mtume wa Mwenyezi SAW akiwa na sisi, tukitoa kwa mtoto na mkubwa, huru na mtumwa katika vyakula vya aina tatu: Pishi moja ya tende, pishi moja ya maziwa makavu, pishi moja ya ngano mbichi" hatukuacha kufanya hivyo mpaka alipokuja Muawiya: "Akaona kuwa vibaba viwili vya ngano ni sawa sawa na pishi moja ya tende"[2].

Imepokelewa kutoka kwa Imamu Bukhari ndani ya Sahihi yake kutoka kwa Muadh Ibn Jabal RA kuwa alisema kuwaambia watu wa Yemen: "Nipatieni nguo – au cha kuvaliwa – katika Zaka sehemu ya ngano na mahindi ni vyepesi kwenu na bora kwa Maswahaba wa Mtume SAW huko Madinah"[3].

---

(1) Maelezo haya yanapatikana kwenye Sahihi Muslimu – Kitabu cha Zaka, mlango wa Zaka ya Fitri kwa Waislamu, ikiwa ni pamoja na tende na ngano, Hadithi namba 985.

(2) Sunani ya Ibn Maja – Mlango wa Sadaka ya Fitri 3/183,

(3) Sahihi Bukhary – Kitabu cha mambo ya Zaka, mlango wa maelezo katika Zaka.

Asili katika Sadaka ni kumtosheleza mtu masikini na kufikia masilahi yake, ikiwa wasomi wanasisitiza kuwa pale patakapo kuwa na masilahi ndio mwelekeo wa Sharia ya Mwenyezi Mungu, kwa kulinganisha ambapo kuna masilahi kwa masikini katika Zaka ya Fitri inakuwa ndio bora hata kama hali ya kuchukua na mazingira ya wakati yanapelekea kipaombele kuwa ni chakula basi kitakuwa ni hicho, ikiwa hali ya masikini na mazingira ya wakati yanapelekea masilahi ni katika thamani au pesa basi na iwe hivyo.

Na huyu ni Muawiyah Ibn Abi Sufyan RA anafanya nusu pishi vibaba viwili vya ngao mbichi ni sawa na pishi moja ya tende, anafanya thamani ndio msingi wa kutoa Zaka, lau isingekuwa thamani ni yenye kuzingatiwa kwake basi asingefanya nusu ya pishi moja ya ngano mbichi ni sawa na pishi moja ya tende ikawa sawa na ikawa inatosheleza.

Na huyu hapa Swahaba Muadhi Ibn Jabali RA anaangalia masilahi ya mwenye kupewa na

kuchukua, anakubali kwa watu wa Yemen nguo badala ya mahindi na ngano, na anamalizia kwa kauli yake: Hiyo ni wepesi kwenu na yenye manufaa zaidi kwa Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW huko Madinah, hivyo akachunga zaidi masilahi yanayozingatiwa na makusudio makuu, naye ni katika Maswahaba katika rai elimu jitihada na mtazamo.

Alikuwa Abu Yusuf [1] mfuasi wa Abi Hanifa RA anasema: Unga wa ngano ninaupenda zaidi kuliko ngano mbichi, na pesa naipenda zaidi kuliko unga wa ngano na ngano mbichi, kwa sababu pesa ipo karibu zaidi kukidhi hitaji la masikini.

---

(1) Naye ni Yakob Ibn Ibrahim Ibn Habib Al-Ansary Al-Kuufy Al-Baghdady, ni mtu wa Imamu Abi Hanifah, alizaliwa huko Kuufah mwaka wa 113H, alikuwa ni mwanachuoni msomi miongoni mwa wahifadhi wa Hadithi, naye ndio wa kwanza kusambaza madhehebu ya Abu Hanifa, na wa kwanza aliyeitwa ﴿Kadhi wa Makadhi﴾ na wa kwanza aliyetengeneza kitabu cha misingi ya fiqih, miongoni mwa vitabu vyake: Al-Kharaaj, na Al-Aamaaly katika fiqih ya madhehebu ya Abi Hanifah, alifariki mwaka 182H. kitabu Al-Iilaam cha Zarkaly 8/193,

Wanachuoni wamesema katika kutoa Zaka ya Fitri ni chakula kinachotumika sana sehemu husika, inawezakuwa chakula maarufu na kutumika sana nchini au sehemu husika si katika aina hizo zilizotajwa kwenye Hadithi, hivyo baadhi ya nchi au maeneo chakula kinachotumika sana kwao ikawa ni unga wa ngano, na baadhi ya nchi zengine au sehemu zengine chakula kinachotumika sana kwao ikawa ni mahindi, baadhi ya maeneo mengine ikawa chakula chao zaidi ni mbunga, hivyo kauli ya wanachuoni waliposema chakula maarufu nchini na kuliwa sana lengo ni kurahisisha kwa mwenye kutoa Zaka ya Fitri, na wakati huo huo kuchunga masilahi ya masikini, kama vile kauli ya Swahaba Muadh kwa watu wa Yemen: Hizo ni nyepesi kwenu na zina manufaa zaidi kwa Maswahaba wa Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW Madinah.

Mwenye kuzingatia uhalisia ndani ya zama zetu na maeneo yetu na wakati wetu huu tulionao ataona kuwa kutoa thamani mara nyingi sana ndio

yenye manufaa zaidi kwa masikini, kwani anakuwa na uwezo wa kufanya matumizi mengi kupitia pesa naye masikini ndiyo mwenye kufahamu zaidi haja zake na mahitaji yake, kama vile zaka pindi masikini atakapo kusanya nafaka nyingi – mpunga au unga wa ngano au ngano mbichi – mara nyingi anakimbilia kwenye kuuza hizi nafaka kwa nusu ya thamani yake au wakati mwengine chini ya nusu ya thamani, jambo ambalo linaakisi vibaya kwenye masilahi ya masikini, mtazamo wetu ni kuwa thamani ina manufaa zaidi kwa masikini ndani ya zama zetu hizi, na kwa hoja hiyo sisi hatupingi kutoa Zaka ya Fitri katika aina za chakula zilizotajwa kwenye Hadithi ya Mtume SWA, na kwa mwenye kwenye aina zengine za chakula au nafaka kwa kulinganisha na kitendo cha Swahaba Muawiyah Ibn Abi Sufyan RA na kupitisha jopo la Wanachuoni, wala mwenye kutoa thamani kwani amri ni upana wa manufaa, hakuna kupinga katika yaliyotofautiana kati ya Wanachuoni wanaozingatiwa na kanuni: "Hakika linapingwa Lililokubaliwa wala halipingwi lenye tofauti".

## MFANO WA TANO

## UFAHAMU WA HADITHI ZA UCHINJAJI

Kutoka kwa Salamah Ibn Al-Ukuui RA amesema: Amesema Mtume SAW: ﴿Mwenye kuchinja miongoni mwenu basi kisibakie chochote nyumbani kwake baada ya chakula cha siku tatu﴾, ulipofika mwaka uliofuata wakasema: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu je tufanye kama tulivyofanya mwaka jana? Akasema: "Kuleni lisheni na hifadhini, kwani mwaka uliopita ulikuwa ni mwaka wa shida kwa watu, hivyo nikataka muwasaidie masikini" (1).

Kutoka kwa Abi Said Al-Kkhudry RA amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW:

(1) Hadithi inaptikana kwenye Sahihi ya Imamu Bukhary – Kitabu cha uchinjaji, mlango wa kinacholiwa katika nyama ya mnyama anayechinjwa na kile kinachozidia, Hadithi namba 5569.

"Musile nyama ya mnyama muliochinja kwa ajili ya Eid ya kuchinja (Udhuhiya) zaidi ya siku tatu" wakalalamika kwa Mtume SAW kuwa wao wana watoto majirani wafanya kazi, akasema Mtume SAW: Kuleni lisheni na hifadhini" [1].

Kutoka kwa Abdillah Ibn Waaqid amesema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu amekataza kula nyama ya udhuhiya baada ya siku tatu", akasema Abdillah Ibn Abibakri: Nikamwambia hayo Amrah akasema: Amesema kweli, kwani nimemsikia Bibi Aisha RA anasema: Wageni kutoka vijijini walikuwa wanakuja mjini zama za Mtume SAW wakifuata nyama za wanyama wanaochinjwa siku za sikukuu ya mfungo tatu. Mtume SAW akasema: Hifadhini nyama za kula siku tatu, kisha toeni sadaka iliyobakia, ilipokuwa baada ya hapo wakasema: Ewe

(1) Hadithi inapatikana kwenye Sahihi Muslimu – Kitabu kuchinja, malango wa maelezo yaliyokuwa yamekatazwa kula nyama baada ya siku tatu mwanzoni mwa Uislamu, na maelezo ya kufutwa kwa amri hiyo na kuhalalisha kwa wakati wowote anaotaka. Hadithi namba 1973.

Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW watu wanatengeneza vibuyu vya kuhifadhia maji kwa ngozi ya wanyama wao na kuyayusha mafuta ya wanyama na kuyahifadhi kwa matumizi ya baadaye. Mtume SAW akawauliza kwani nani amewazuia kufanya hivyo? Wakasema: Umekataza kula nyama ya wanyama hawa wa udhuhiya baada ya siku tatu, akasema Mtume SAW: Kwa hakika nilikukatazeni ni kwa sababu ya misafara ya watu wanaokuja kutoka vijijini kuja kufuata misaada, hivyo basi kuleni na hifadhini pia toeni sadaka" (1).

Kutoka kwa Ibn Omar RA kuwa Mtume SAW amesema: "Mmoja wenu asile nyama ya udhuhiya zaidi ya siku tatu" (2).

---

(1) Hadithi imo kwenye Sahihi Muslimu – Kitabu cha mambo ya kuchinja, mlango wa maelezo yaliyokuwa yamekatazwa kula nyama za wanyama wa udhuhiya baada ya siku tatu wakati wa mwanzo wa Uislamu, na maelezo ya kuondolewa kwa katazo hilo na kuhalalishwa kwa wakati wowote mtu autakao. Hadithi namba 1971.

(2) Sunani ya Tirmidhy – Kitabu cha mambo ya kuchinja kwa Mtume SAW, mlango wa chukizo la kula nyama ya udhuhiya zaidi ya siku tatu. Hadithi namba 1509.

Kupitia kusoma kwetu mwenendo wa Hadithi hizi na mnasaba wa kila Hadithi inatuwea wazi kuwa Hadithi "Kuleni na toeni sadaka na hifadhani" na Hadithi "Musile nyama ya udhuhiya zaidi ya siku tatu" haijafutwa Hadithi yeyote katika hizo, lakini kila moja katika hizo ilikuwa kwenye hali maalum, ambapo katika hali ya ustawi na nafasi zaidi basi hufanyiwa kazi kauli ya Mtume SAW: "Kuleni na toeni sadaka na hifadhini». Na inapokuwa hali ya shida kwa watu hufanyiwa kazi kauli ya Mtume SAW: "Mmoja wenu asile nyama ya udhuhiya zaidi ya siku tatu" hivyo baada ya Mtume SAW kuwakataza kula nyama zaidi ya siku tatu walimuuliza ndani ya mwaka uliofuata, Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu ulikuwa umetukataza kula nyama ya udhuhiya kwa zaidi ya siku tatu. Mtume SAW akasema: "Kuleni lisheni na hifadhini, kwani mwaka huo watu walikuwa kwenye shida zaidi nikataka muwasaidie".

Watu wengi wanasimamia kauli ya Mtume SAW: "Kuleni na lisheni na toeni sadaka» na wanaanga-

lia kinachofanana na utakatifu kauli za baadhi ya Wanachuoni kwa kugawa nyama ya udhuhiya sehemu tatu: Theluthi moja kwa ajili ya masikini, theluthi nyengine ya kutoa kama zawadi, theluthi nyengine ni kwa ajili ya mtu mwenyewe na familia yake, kuwa mgawanyo huu ni kitendo cha matumizi ya ukaribu, na kusudio lake lilikuwa ni kutofaa kwa mchinjaji kula fungu la masikini, na kuwahusisha angalau theluthi moja ya mnyama wake, lakini mwenye kuzidisha basi Mwenyezi Mungu atamzidishia fadhila zake.

Lakini watu wengi wanajisahau kuwa Mtume SAW pindi alipowaona watu wanashida aliwaambia: "Yeyote miongoni mwenu mwenye kuchinja basi wala isiwe nyama nyumbani kwake zaidi ya siku tatu, ulipokuja mwaka mwengine Maswahaba wakauliza: Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu je tunafanya kama tulivyofanya mwaka uliopita? Mtume SAW akasema: Kuleni, lisheni, hifadhini, kwani mwaka huo uliopita watu walikuwa na kipindi kigumu hivyo nikataka muwasaidie", pindi

kunapokuwa na hali nzuri hufanyiwa kazi kauli ya Mtume SAW: "Kuleni toeni sadaka na hifadhini﴾, pindi watu wanapokuwa na shida na mahitaji zaidi hufanyiwa kazi kauli ya Mtume SAW: "Yeyote miongoni mwenu mwenye kuchinja basi isibakie nyama nyumbani kwake zaidi ya siku tatu".

Hivyo tunasisitiza juu ya umuhimu wa kuwasidia watu masikini na wenye kuhitaji pamoja na kuwakirimu kwa fungu lenye kutosheleza la nyama ya udhuhiya, pindi alipouliza Mtume wetu SAW kumuuliza Bibi Aisha R.A pindi walipochinja mnyama na kusema: "Je kuna kilichobakia?" akasema: Hakuna kilichobakia isipokuwa kidogo. Akasema Mtume SAW: Inayobakia ni yote na wala sio sehemu yake (1), kwani kinachotolewa sadaka ndio ambacho anakihifadhi mwanadamu na kukikuta ambapo Mwenyezi Mungu Anasema: ﴿**Mulivyo navyo vitakwisha na vilivyoko kwa Mwenyezi Mungu ndivyo vitakavyo bakia**﴾(2).

(1) Sunani Tirmidhy – Kitabu cha ndoa. Hadithi namba 2470.
(2) An-Nahl: 96.

Mtume wetu SAW ametuhimiza siku za Eid kuwasaidia watu mafakiri na masikini, akasema Mtume SAW: 'Watoshelezeni ndani ya siku hii" [1], kwa maana wapeni na wakidhieni mahitaji yao wala asilazimike yeyote miongoni mwao kuanza kuomba ndani ya siku hii, kwani neema huongezeka kwa kushukuru, na huondoka kwa kukufuru, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema: ﴿**Na alipo tangaza Mola wenu Mlezi: Mukishukuru nitakuzidishieni, na mukikufuru, basi adhabu yangu ni kali**﴾[2]. Na Anasema Mola Mtukufu: ﴿**Angalieni! Nyinyi munaitwa mtumie katika njia ya Mwenyezi Mungu, na wapo katika nyinyi wanao fanya ubahili. Na anaye fanya ubahili basi anajifanyia ubahili mwenyewe. Na Mwenyezi Mungu si muhitaji, na nyinyi ndio wahitaji. Na mukigeuka atawaleta watu wengine badala yenu, nao hawatakuwa kama nyinyi**﴾[3].

(1) Sunan Ad-Dar Qutwniy – Kitabu cha Zaka ya Fitri. Hadithi namba 2133.
(2) Ibrahimu: 07.
(3) Muhammad: 38.

Na anasema Mtume wetu Muhammad SAW: "Hakuna siku ambayo watu wanakuwa isipokuwa Malaika wawili huteremka, mmoja anasema: Ewe Mwenyezi Mungu mpe malipo mema kwa alichokitanguliza, na mwengine anasema: Ewe Mwenyezi Mungu muharibia mali zake kwa mwenye kujizuia kuitoa"[1], na anasema Mtume SAW: "Hakika Mwenyezi Mungu huwapa neema ambao wanashuhurishwa na mahitaji ya watu wengine, madamu hawatashikilia ikiwa watazishikilia huamishwa kutoka kwao na kupewa wengine"[2].

***

(1) Hadithi imo kwenye Sahihi Bukhary – Kitabu cha mambo ya Zaka, mlango wa kauli ya Mwenyezi Mungu: ﴾Ama mwenye kutoa na kumcha Mungu kisha akasadikisha vizuri basi tutamrahisishia kwenye wepesi﴿ Hadithi namba 1442.

(2) Muujamu Al-Ausatw 8/186. Hadithi namba 8350 chapa ya Dar al-Haramain. Kairo.

## MFANO WA SITA

### UELEWA WA HADITHI ZA KUSIMAMA.

Kutoka kwa Muadhi RA amesema: Nimemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW anasema: "Mwenye kupenda watu kumsimamia, basi na ajiandae makazi yake motoni"(1).

Kutoka tena kwa Muadhi RA amesema: Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW: "Mwenye kupenda kusimamiwa na waja wa Mwenyezi Mungu basi na aandae nyumba motoni"(2).

Kutoka kwa Abi Umama RA amesema: Alitujia Mtume wa Mwenyezi Mungu SAW akiwa mwenye

(1) Sunani ya Abi Daud – Kitabu cha Adabu, mlango mtu kumsimamia mtu mwengine. Hadithi namba 5229.

(2) Kitabu cha Adabu al-Mufrad cha Imamu Bukhary – Mlango wa mtu kusimsimamia mtu kwa kumtukuza, ukurasa wa 339 Hadithi namba 5229.

kuiegemea fimbo, tukasimama, akasema: "Musisimame kama wanavyosimama Wafursi wanavyotukuzana wao kwa wao"(1).

Kutoka kwa Abi Said RA amesema: Watu wa Quraidhah walipinga hukumu ya Saad Ibn Muadh. Mtume SAW alimtuma mjumbe kwake akaja na akasema: "Wasimamieni viongozi wenu au akasema: Wabora wenu. Saad alipokaa mbele ya Mtume SAW akaambiwa: Hawa wamepinga hukumu yako, akasema: Hakika nimehukumu kupigwa wapiganaji wao na kuachwa wanawake wao na watoto wao. Mtume SAW akasema: Kwa hakika umehukumu vile alivyohukumu Mfalme wa mbingu na ardhi"(2).

Kutoka kwa Anas RA kuwa Maswahaba wa Mtume SAW walikuwa pindi wanapokutana wana-

---

(1) Sunani Abi Daud – Kitabu cha Adabu, mlango wa mtu kumsimamia mtu mwengine. Hadithi namba 5230.

(2) Sahihi Bukhary – Kitabu cha kutaka ruhusa, mlango wa kauli ya Mtume SAW: ﴿Wasimamieni viongozi wenu﴾. Hadithi namba 6262.

peana mikono, na wanaporudi kutoka safari basi hukumbatiana [1].

Ambalo tunalifahamu kutokana na Hadithi hii ni kuwa kukataza kusimama sio kila kusimama, bali ni kusimama kwa kumtukuza mtu kama walivyokuwa wanafanya Wafursi, kuzuia kulikokuja kunachukuliwa kusimama kwa kutukuza, hilo kama lilivyoelezewa na upokezi uliokuja: "Musisimame kama wanavyosimama Wafursi wakitukuzana wao kwa wao" amefasiri Imamu Bukhary RA kwenye Kitabu chake cha Adabu al-Mufrad kwa kauli yake: "Mlango wa mtu kumsimamia mtu mwengine kwa kumtukuza", nayo ndio fasiri iliyofasiriwa na Abu Daud pia katika Kitabu chake kwa kusema: Mlango wa mtu kumsimamia mtu mwengine anafanya hivyo kwa kumtukuza.

Katika yanayosisitizwa ni kuwa kusimama kulikokatazwa ni kule kusimama kwa kutukuza na

(1) Kitabu cha Muujamu Al-Ausat cha Twabrany Hadithi namba 97, na kukumbatiana hakuwi isipokuwa ni kwa kusimama.

wala sio kusimama tu kwa kauli ya Mtume SAW: "Wasimamieni viongozi wenu" kwa maana ya Saad Ibn Muadh RA, ingekuwa kusimama kumekatazwa moja kwa moja basi Mtume SAW asingesema: "Wasimamieni viongozi wenu» kisha maelezo ya Mtume SAW: "Mwenye kupenda kusimamiwa na watu» yanaashiria kwa mwenye kujiona nafsi yake ukubwa unaopaswa watu wamsimamie kwa kumtukuza na utukufu, lakini ikiwa watu watamsimamia kwa upendo wao na kutambua kwao akiendana na hali ya unyenyekevu na hofu kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mtukufu basi hakuna ubaya ndani yake.

***

# Vyanzo Muhimu na Marejeo.



| | |
|---|---|
| 01 | Al-Ihkaam fii Usuul al-Ahkaam cha Ibn Hazm Ad-Dhaahiry, Dar al-Aafaaq al-Jadidah – Beirut. |
| 02 | Al-Ihkaam fii Tamyiiz al-Fataawa an Ahkaam cha Imamu Al-Quraafy, Dar Al-Bashaair Al-Islaamiyah ya uchapishaji na usambazaji Beiruti – Lebanon. |
| 03 | Al-Ikhtiyaar Litaalil al-Mukhataar, cha Ibn Mauduud Al-Hanafy (Amefariki mwaka 683H), Dar al-Maarifah. |
| 04 | Al-Aadab Shariiyah cha Ibn Muflih Al-Maqdasy amefariki: 763H, kinasambazwa na Dar Aalam al-Kutub. |
| 05 | Al-Adab Al-Mufrad cha Imamu Bukhary, uhakiki umefanywa na: Muhammad Fuad Abdulbaaqy, Dar al-Bashaair Al-Islaamiyah, Bairut. |

| | |
|---|---|
| 06 | Irshaad Al-Fuhuul ilaa Tahkiik al-Hakki min Ilmu al-Usuul cha Shaukaany, Dar al-Kitaabu Al-Araby. |
| 07 | I'ilaamu al-Muwaqqeen ani rabbu al-Aalameen cha Ibn Qayyim Al-Jauzy, kimefanyiwa uhakiki na: Twaha Abdulrauuf, chapa ya Dar al-Jambaly – Beirut. |
| 08 | Al-A'alaam cha Kheir Deen Zarikaly (aliyefariki mwaka 1396H) Usambazaji: Dar al-I'lmu lil malaayeen. |
| 09 | Al-Itiqaan fii uluum Al-Quran cha Imamu As-Suyuutwy (aliyefariki mwaka 911H) uhakiki umefanywa na: Muhammad Abulfadhli Ibrahim, usambazaji: Taasisi kuu ya vitabu nchini Misri. |
| 10 | Al-Ifswaah an maan as-Swahhah cha Ibn Hubeirah Ad-Dhihly As-Shaibany (amefariki mwaka: 560H) uhakiki: Fuad AbdulMuneem Ahmad, chapa ya Dar al-Watwan. |
| 11 | Al-Ummu cha Imamu Shaafy, chapa ya Dar Al-Maarifah – Beirut. |

| | |
|---|---|
| 12 | Badaai'I As-Swanaai'I fii tartiibu as-Sharaai'I, cha Abibakri Ibn Masuud Ibn Ahmad al-Kaasaany (amefariki mwaka wa 587H) chapa ya Dar al-Kutubu al-Ilmiya – Beirut. |
| 13 | Tuhfah al-Ahwadhy sherehe ya Jaamii Tirmidhy, Dar al-Kutub al-Ilimiya – Beirut. |
| 14 | Jaami'I al-uluum wal hikam cha Ibn Rajab Al-Hambaliy chapa ya Dar al-Maarifah – Beirut. |
| 15 | Ar-Risaalah cha Imamu Shaafy, uhakiki umefanywa na: Sheikh Ahmad Shaakir, Dar al-Kutub al-Ilmiya – Beirut. |
| 16 | Rasaail Ibn Aabideen cha Mwanachuoni Muhammad Ameen Afandy maaurufu kama Ibn Aabideen, uhakiki umefanywa na: Muhammad Al-Azaazy, Dar al-Kutub al-Ilmiyah – Beirut. |
| 17 | Ruuh al-Maany fii tafsiri Al-Quran al-Adheem wa As-Sab'uu al-Mathaany cha Aaluusy, Dar Ihyaau at-Turaath Al-Araby – Beirut. |
| 18 | Sunan Ibn Majah chapa ya: Dar ar-Risaalah al-A'alamiyah. |

| | |
|---|---|
| 19 | Sunan Abi Daud, uhakiki umefanywa na: Muhammad Muhyideen Abdulhameed, usambazaji: Maktabatu al-A'sriyah, Saidah – Beirut. |
| 20 | Sunan Tirmidhiy, uhakiki na maelezo: Ahmad Muhammad Shaakir, usambazaji: Shirika Maktabat na uchapishaji Mustafa Al-baby Al-Halaby Cairo. |
| 21 | Sunan Dar Qutwuny, chapa ya: Taasisi ya Ar-Risaalah – Beirut – Lebanon. |
| 22 | As-Sunan al-Kubraa cha Baihaqy, Dar al-Kutub Al-Ilmiyah – Beirut – Lebanon. |
| 23 | Seir A'alaam An-Nablaa cha Shams Deen Ad-Dhahby (amefariki mwaka wa 748H), uhakiki: Sheikh Shuaib Al-arnaauutw, usambazaji: Taasisi ya Risaalah – Beirut. |
| 24 | Shadhraat Ad-Dhahab fii akhbaar min dhahabi cha Ibn Al-A'mmaad Al-Hambaly (amefariki mwaka 1089H), usambazaji: Dar Ibn Katheer. Damascus – Beirut. |

| | |
|---|---|
| 25 | Sherhu An-Nawawy alaa Swahiih Muslimu, usambazaji: Dar Akhbaar at-Turaath Al-Araby – Beirut. |
| 26 | Shaabul Iimaan cha Baihaqy, Dar al-Kutub al-Ilmiyah – Beirut. |
| 27 | Sahiih Al-Bukhary, uhakiki: Muhammad Zuheir Ibn Nassor, usambazaji: Dar Twauq An-Najaat – Beirut – Lebanon. |
| 28 | Sahiih Muslimu, uhakiki: Muhammad Fuad Abdulbaaqy, usambazaji: Dar Ihayaau at-Turaath Al-Araby – Beirut. |
| 29 | Twabaqaat Shaafi'iyah al-Kubraa, Taajuddeen Abdulwahaab Ibn Taqiyyudeen As-Sabaky (amefariki mwaka wa 771) kimefanyiwa uhakiki na: Dr. Muhammad Twanaahy, usambazaji, Dar Hijri ya uchapishaji na usambazaji. |
| 30 | Twarhu Tathreeb fii sherhi taqreeb cha Zeinudeen A-Iraaqy, chapa ya Kimisri. |
| 31 | I'lmu Usuul Al-Fiqhi. Abdulwahaab Khalaaf, chapa ya: Matbaatu al-Madany nchini Misri. |

| | |
|---|---|
| 32 | Fat'hul baary sherhu Sahiih Al-Bukhary cha Ibn Hajar Al-Asqalaany, usambazaji: Dar al-Maarifah – Beirut. |
| 33 | Qawaa'id al-ahkaam fii maswaalih al-anaam cha Abi Muhammad Ezzuddeen Ibn Abdulsalaam, chapa ya: Dar al-maarif – Beirut. |
| 34 | Lisaanu Al-Arabu cha Ibn Mandhuur (amefariki mwaka wa 711H) Dar Swaadir – Beirut. |
| 35 | Al-Mustadriku alaa Swahiihain cha Hakim, Dar al-Kutub al-I'lmiyahh – Beirut. |
| 36 | Al-Mustaswfy cha Abi Haamid Al-Ghazaly, uhakiki: Muhammad Abdulsalaam Abdulshaafy, Dar al-Kutub al-I'lmiyah – Beirut. |
| 37 | Al-Mustaswfy min I'lmi al-Usuul cha Ghazaly. Dar al-Kutub al-I'lmiyah – Beirut. |
| 38 | Musnad Imam Ahmad, chapa ya Taasisi ya Risaalah. |

| | |
|---|---|
| 39 | Musnad Al-Bazzar cha Abibakri Ahmad Ibn Amru Al-Atakiy maarufu kwa jina la Bazzar (amefariki mwaka wa 292) uhakiki: Mahfudh Al-Rahman Zeinullah, usambazaji: Maktabatu al-Uluum wal hikam – Madinatul Al-munawwarah. |
| 40 | Al-mu'ujam al-ausat cha Twabraany, chapa ya: Dar Al-Haramain. Cairo. |
| 41 | Al-muujam al-ausat, utunzi / Ibrahim Mustafa – Ahmad Zayyat – Haamid Abdulqaadir – Muhammad Najjaar, uhakiki: Jopo la wanalugha ya Kiarabu. Cairo. |
| 42 | Maqaaswid al-Hassanat cha Sakhaawiy, chapa ya: Dar al-Kutub Al-Araby. |
| 43 | Al-Muhaddhib fii Fiqhi ya Imamu Shaafy cha Abi Is-haaq Sheerazy (amefariki mwaka wa 476H) chapa ya: Dar al-Kutub al-I'lmiyah – Beirut. |
| 44 | Al-muwaafaqaat cha Imamu Shaafy, Dar Ibn Affaan, chapa ya kwanza. |

| | |
|---|---|
| 45 | An-Nihaayay fii ghareeb al-hadath wal athar, cha Ibn Atheer (amefariki mwaka wa 606H) uhakiki: Twahar Ahmad Zaawiy, chapa ya: Maktabat al-I'lmiyah – Beirut. |
| 46 | Nail al-autwaar cha mwanachuoni Muhammad Ibn Ally Ibn Muhammad Ibn Abdillah Shaukaany Myemen (amefariki mwaka wa 1250H) usambazaji: Dar al-Hadith. Cairo. |

## Kurasa za Maudhui.


| | |
|---|---|
| Utangulizi | 5 |
| Utafiti wa Kwanza: Mazungumzo ya Quran kuhusu Mtume SAW. | 13 |
| Utafiti wa Pili: Nafasi ya Sunna na hoja zake | 29 |
| Utafiti wa Tatu: Umuhimu wa mitazamo mipya. | 57 |
| Utafiti wa Nne: Maudhui ya ujumbe wa Uislamu na umuhimu wa uelewa wa makusudio yake | 77 |
| Utafiti wa Tano: Mfumo wa Ibada na Desturi za matendo. | 89 |
| Utafiti wa Sita: Matendo ya Mtume SAW katika kuendesha nchi. | 99 |
| Utafiti wa Saba: Mifano ya kiutendaji ya ufahamu wa makusudio ya Sunna ya Mtume. | 105 |

Mfano wa Kwanza: Uelewa wa Hadithi za upigaji mswaki. 105
Mfano wa Pili: Uelewa wa Hadithi za usafi wa kitanda. 109
Mfano wa Tatu: Uelewa wa Hadithi za kushusha nguo chini. 117
Mfano wa Nne: Uelewa wa Hadithi za Sadaka ya Fitri. 127
Mfano wa Tano: Uelewa wa Hadithi za uchinjaji Udhuhiya 137
Mfano wa Sita: Uelewa wa Hadithi za kumsimamia mtu. 145

Vyanzo Muhimu na Vitabu vya Marejeo. 149

Shirika Kuu la Vitabu la Misri.

Msimamizi wa miradi ya kitamadani.

**Marwan Hamad**

**Mkaguzi**

**Faryal Fuad**

Mtangenezaji wa jarada la kitabu

**Muhammad Baghadady**

**Upande wa Ufundi**

**Mirfat Antar An-Nuhas**

Namba ya kuhifadhia kwenye kitengo cha vitabu 2021

SIBN